AL-AZHAR UNIVERSITY
BULLETIN OF THE FACULTY
OF
LANGUAGES & TRANSLATION

جامعة الأزهر
مجلة كلية اللغات والترجمة

# Uchunguzi wa muktadha wa tamthilia za kielemu kuhusu "UKIMWI"

**By**

**Dr. Gehan Mustafa Al-Qadi**

***Department of African Languages, Faculty of Al-Alsun***
***Ain-Shams University, Cairo, Egypt***

**A contextual analysis of educational plays about HIV/AIDS**

Gehan Mustafa Al-Qadi
Department of African Languages, Faculty of Al-Alsun, Ain-Shams University, Cairo, Egypt
Email: Jehan.Elqadi@alsun.asu.edu.eg

**ABSTRACT:** Illness represents a unique emotional state experienced by the patient, placing them in a complex blend of fear, pain, and anticipation of the future. This intricate emotional experience affects not only the individual but also the wider society. Literature, in its various forms, expresses this impact depending on how the illness manifests—whether as a widespread epidemic, a condition confined to a specific group, or an individual case representing a personal experience.

Throughout history and across different societies, literature has addressed such phenomena, particularly during times of epidemics and public health crises. Given its inherent nature of shedding light on social problems and human suffering, literature plays a key role in highlighting various aspects of such crises—whether from an educational perspective aimed at raising awareness, a psychological one that reveals the inner state of the patient, or a social lens that uncovers the broader societal consequences.

In this study, we focus on epidemic literature taught in schools, specifically works that address AIDS in Tanzania through a collection of plays studied by students. These plays serve as an educational tool to raise awareness and combat this deadly epidemic, which continues to spread across the African continent.

**Keywords: AIDS – Disease Literature – School Literature – Historical Context – Social Context – Psychological Context.**

**تحليل سياقي للمسرحيات التعليمية المتعلقة بفيروس نقص المناعة البشرية/الإيدز**

جيهان مصطفى القاضى
قسم اللغات الأفريقية، كلية الألسن جامعة عين شمس، القاهرة، مصر
البريد الإلكتروني: Jehan.Elqadi@alsun.asu.edu.eg

**ملخص:** يمثل المرض حالة شعورية خاصة يعيشها الإنسان المريض ويجعله في مزيج ما بين الخوف والألم وترقب المستقبل؛ هذا المزيج من الشعور الإنساني المركب ينتج عنه تأثير على الفرد والمجتمع، ويعبر عنه الأدب بأشكاله المختلفة وفق تأثير هذا المرض على المجتمع إن كان مرض وبائي أو مرض خاص بطائفة معينة أو مرضا شخصيا يمثل حاله فردية، وقد تناول الأدب هذه الظواهر في أدبياته الإنسانية عبر العصور وفي مجتمعات المختلفة وخاصة في أوقات الأوبئة والجوائح الصحية، فبطبيعية الأدب الذي يلقي الضوء على أي مشكلة اجتماعية أو أزمة إنسانية يتجلى دوره في توضيح جوانب هذه الأزمة أما من منظور توعوي أو من منظور نفسي بإظهار حالة المريض أو حتى من منظور اجتماعي بغرض توضيح الآثار الاجتماعية المترتبة، ونحن هنا في هذا البحث نتناول أدب الأوبئة الذي يدرس في المدارس ويناقش وباء الإيدز في تنزانيا من خلال مجموعة من المسرحيات التي يدرسها الطلاب التنزانيون في المدارس كوسيلة توعوية لمحاربة هذا الوباء الفتاك المنتشر في أفريقية.

**الكلمات المفتاحية: الإيدز- أدب المرض - أدب المدرسة - السياق التاريخي - السياق الاجتماعي - السياق النفسي.**

**Ikisiri:**

Ugonjwa ni hali ya kipekee ya kihisia anayopitia mgonjwa, hali inayomweka katika hofu, maumivu na kusubiri kwa wasiwasi hali ya baadaye. Mchanganyiko huu wa hisia tata za kibinadamu huleta athari kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla, na fasihi huonyesha hali hii kwa namna mbalimbali kulingana na jinsi ugonjwa unavyoathiri jamii – iwe ni ugonjwa wa mlipuko, ugonjwa wa kuambukiza au usioambukiza. Fasihi imekuwa ikishughulikia hali hizi katika maandiko yake ya kwa nyakati tofauti na katika jamii mbalimbali, hasa wakati wa milipuko ya magonjwa na majanga ya kiafya, hivyo fasihi huangazia matatizo ya kijamii au misukosuko ya kibinadamu na kuonyesha vipengele mbalimbali vya hali hizo – iwe ni kwa mtazamo wa kuelimisha, au wa kisaikolojia kwa kuonyesha hali ya mgonjwa, au hata kwa mtazamo wa kijamii kwa lengo la kueleza athari za kijamii zinazotokana na hali hiyo. Katika utafiti huu, tunachambua fasihi maambukizi ya magonjwa inayofundishwa mashuleni, hasa jinsi inavyoshughulikia ugonjwa wa UKIMWI nchini Tanzania kupitia mfululizo wa tamthilia zinazofundishwa kwa wanafunzi wa Kitanzania kama njia ya kuelimisha jamii na kupambana na janga hili hatari linalosambaa kwa kasi barani Afrika.

**Maneno muhimu**: ***UKIMWI, Fasihi ya Maradhi, Fasihi ya kielemu , Muktadha wa Kihistoria, Muktadha wa*** **Kijamii, Muktadha wa Kisaikolojia.**

**Fasihi ya Maambukizi ya Magonjwa:**

Tangu nyakati za kale, ugonjwa umetumika kama taswira ya uovu katika kazi za kifasihi, kama inavyoonekana katika tamthilia ya Oedipus Mfalme ya mwandishi Sophocles. Hata hivyo, baadaye ugonjwa ukawa mhimili wa kipekee na msingi katika ujenzi wa kazi ya kifasihi, na hivyo kuzaliwa kwa tawi maalum la fasihi lijulikanalo kama fasihi ya magonjwa. Hii ilijitokeza wazi wakati wa kuenea kwa ugonjwa wa tauni, ambapo theluthi ya watu duniani walifariki kwa ugonjwa huo bila kugunduliwa tiba, na wachache tu ndio walionusurika. Hali hii iliwasisimua waandishi kuandika kazi za fasihi zinazoonyesha mateso anayopata binadamu kutokana na ugonjwa, dalili zake, mazingira ya kuambukizwa, na juhudi za kutafuta suluhisho au namna ya kujikinga.Hivyo basi, fasihi ya magonjwa ikawa jina mahsusi la kazi za aina hii, ambazo huzingatia hali za magonjwa kama kiini cha simulizi. Katika enzi za kati barani Ulaya, ugonjwa wa tauni ulisambaa kwa kiwango cha kutisha, na kuua maelfu ya watu, hali iliyozua kazi mbalimbali za kifasihi zilizoelezea athari mbaya za ugonjwa huo. Mojawapo ya kazi za zamani kabisa za kifasihi kuhusu mlipuko huo ni Decameron, mkusanyo wa hadithi kutoka kwa mwandishi wa Kiitaliano Giovanni Boccaccio, inayohusu watu kumi waliokimbia jiji la Florence kuokoa maisha yao dhidi ya tauni, wakieleza hadithi za kejeli

zinazoonyesha madhila kwa jamii yao. (Boccaccio, 2006, pp. 7–8) Katika enzi za kati pia kwa Waarabu, ugonjwa wa tauni ulienea kwa kiwango kikubwa, na ulihusishwa moja kwa moja na kuanguka kwa Dola ya Umawiyya, kama ilivyoelezwa katika kitabu Tauni katika Enzi ya Umawiyya cha Ahmad Al-Adawi. (Al-Adawi, 2013) Aidha, kazi nyingi za kifasihi za Kiarabu zilizungumzia janga hili, zikiwemo kazi za nathari na mashairi ya Ibn Al-Wardi, ambaye alielezea kwa kina mlipuko wa tauni ulioikumba nchi za Kiislamu na athari zake kwa maisha ya watu. (Shihan, 2022, pp. 136–137)

Hivyo basi, kulizuka aina ya fasihi inayoshughulikia milipuko ya magonjwa kama jambo la kibinadamu linalomkabili binadamu na linalohitaji kupatiwa suluhisho. Magonjwa haya yanachukuliwa kama janga lenye uzito wake, si kama sehemu ya matatizo mengine ya kijamii, bali kama hali ya kipekee ambayo fasihi hujaribu kueleza mazingira yake, athari zake, njia za kujikinga nayo, na wakati mwingine hata njia za matibabu.

Fasihi hii imeendelea kuwepo hadi nyakati za sasa, na huenea kwa wingi hasa wakati wa milipuko na majanga ya kiafya. Miongoni mwa kazi mashuhuri za kifasihi za kisasa zilizoshughulikia ugonjwa wa tauni ni riwaya The Plague (Tauni) ya Albert Camus, mmoja wa waandishi walioguswa sana na janga hili, akiielezea katika muktadha wa kuenea kwake nchini Algeria – nchi yake ya asili. Hali hiyo pia imeonyeshwa katika tamthilia yake ya State of Siege , inayosimulia kuhusu jiji lililokumbwa na mlipuko kama huo.

Hata hivyo, ugonjwa wa tauni haukuwa wa pekee katika fasihi ya magonjwa, kwani pia ugonjwa wa mafua ya mwaka 1918 ulielezewa katika riwaya Pale Horse, Pale Rider ya mwandishi wa Kimarekani Katherine Anne Porter, iliyochapishwa mwaka 1939, inayozungumzia mlipuko ulioua maelfu ya Wamarekani. (Porter, 2023) Katika fasihi ya magonjwa ya Magharibi ya kisasa, ugonjwa wa saratani ulishughulikiwa kwa kina kama ugonjwa wa zama hizi. Mfano ni tamthilia The Shadow Box ya Michael Cristofer, ambayo inasimulia maisha ya watu watatu waliopata saratani, changamoto wanazokumbana nazo, mazungumzo yao, na hisia wanazopitia wanapokabiliana na hatima yao. (Cristofer, 1993) Katika fasihi ya Kiswahili, mojawapo ya kazi zinazowakilisha aina hii ya fasihi ni tamthilia Kifo Kisimani ya mwandishi wa Kenya Kithaka wa Mberia, inayosimulia mlipuko wa kipindupindu katika kijiji kimoja cha pwani ya Kenya, na kuonyesha athari za kisaikolojia na kijamii za ugonjwa huo. (Wa Mberia, 2001) Hakuna tafsiri kamili inayokubalika kwa ujumla kuhusu maana ya fasihi ya magonjwa lakini utafiti huu unaeleza kuwa si kila kazi ya fasihi inayotaja ugonjwa inaweza kuhesabiwa kama fasihi ya magonjwa. Ili kazi ihesabiwe kuwa ya aina hii, ugonjwa lazima uwe dhamira kuu katika kazi ya

fasihi, na si tu kuonekana kama hali ya kibinadamu ndani ya hadithi. Kwa sababu magonjwa ni hali ya kawaida katika maisha ya binadamu, mara nyingi huwasilishwa katika fasihi kama mojawapo ya changamoto za maisha. Hali hii imejitokeza katika fasihi ya Kiafrika, Kiarabu na hata Magharibi. Hata hivyo, kazi hizi haziwezi kuhesabiwa kuwa ni sehemu ya fasihi ya magonjwa kwa sababu hazitumii ugonjwa kama msingi wa ujenzi wa kazi yenyewe, bali kama hali ya kawaida ya maisha. Mfano ni riwaya Watoto wa mama ntilie ya Emmanuel Mbogo, ambapo mwandishi anazungumzia kuhusu ugonjwa wa mara kwa mara wa homa na malaria unaompata mhusika mkuu, kifo cha binti yake kutokana na kichaa cha mbwa, na vifo vya mama wa watoto wa mitaani kwa magonjwa mbalimbali, lakini yote haya yanawasilishwa kama sehemu ya maisha ya umasikini na hali duni ya kiuchumi, bila kuwepo kwa matibabu au uwezo wa kwenda hospitalini. (Mbogo, 2002)

Vilevile zipo kazi za fasihi zinazojadili hali za kisaikolojia na kueleza magonjwa ya akili na hisia za mtu kuhusu hali hiyo na upweke wake, pia haziwezi kuhesabiwa kuwa ni fasihi ya magonjwa, kwani huwa zinaegemea zaidi upande wa fasihi ya kisaikolojia ambayo hulenga kuonyesha hisia za mtu katika mazingira hayo. Mfano wa hili ni mkusanyiko wa hadithi fupi za kweli unaoitwa "'The Man Who Mistook His Wife for a Hat and Other Clinical Tales " Kitabu hiki cha mwandishi Oliver Sacks kinaelezea visa vya kitabibu adimu na tata ambavyo alikumbana navyo akiwa daktari wa magonjwa ya akili na neva. Kinazungumzia hali za kiafya zinavyoathiri utendaji wa jumla wa mwili na hisia za binadamu, na jinsi hali hizi zinavyoathiri uzoefu wao wa maisha ya kila siku. (Sacks, 1985)

Mchanganyiko huu hauishii katika aina hizo mbili tu, bali pia unajitokeza katika fasihi ya kisayansi ya kubuni inayozungumzia mada zinazohusu maangamizi ya dunia kupitia milipuko ya virusi visivyojulikana. Kazi kama hizo zinaangukia katika uwanja wa fasihi ya kisayansi ya kubuni, na si fasihi ya magonjwa, ingawa kwa makosa zimewahi kujumuishwa ndani ya fasihi ya magonjwa, wakati ukweli ni kuwa baadhi ni fasihi ya kisayansi ya kubuni au hata ya kufikirika (fantasia). Au kile kinachojulikana kama fasihi ya mwisho wa dunia (Apocalyptic Literature), na mfano maarufu zaidi duniani ni riwaya ya The Stand ya mwandishi Stephen King, ambayo ilitumia dhamira ya ugonjwa wa mlipuko katika muktadha wa kubuni ili kuonyesha maisha baada ya janga hilo kuangamiza sehemu kubwa ya dunia. Waliosalia wanaonekana wakijaribu kutathmini upya maisha yao na kugundua maisha yaliyojaa huruma zaidi baada ya ugonjwa huo kuwaangamiza waovu. Mtindo huu wa kifasihi hauwezi kuhesabiwa kama fasihi ya magonjwa, licha ya kutumia wazo hilo, kwa sababu lengo lake si ugonjwa wenyewe—ambao ni wa kubuni—bali ni kuonyesha maisha baada ya mlipuko huo. (King, 1990)

Kadhalika, fasihi ya Magonjwa inatofautiana na fasihi ya tiba (medical literature) ambayo huandikwa na madaktari wakieleza uzoefu wao binafsi kuhusu magonjwa na wagonjwa, pamoja na hali walizokutana nazo katika mazingira yao ya kazi ya matibabu – kazi hizi huwa ni zaidi ya wasifu wa kimatibabu na si kazi za fasihi ya magonjwa. Kama ilivyo katika riwaya ya This Is Going to Hurt iliyoandikwa na daktari wa Uingereza, Adam Kay, ambayo inaonyesha kumbukumbu zake wakati wa mafunzo yake kama daktari katika hospitali mbalimbali za Uingereza. Riwaya hii inaeleza kuhusu wagonjwa kutoka vitengo tofauti, pamoja na uchovu wa kiakili na shinikizo kubwa analopitia daktari katika kazi yake ya kila siku. (Kay, 2017)

Ikiwa tungependa kuweka mtazamo wa kina kuhusu fasihi ya magonjwa tunaweza kupendekeza kuwa:

tunaondoa kutoka kwenye fasihi ya magonjwa, magonjwa ya akili yanayoonyesha tabia za kisaikolojia kama vile (psychopathy), kwa kuwa hayo huangukia katika fasihi ya kisaikolojia zaidi kuliko fasihi ya magonjwa, pia tunaondoa magonjwa ya kubuni yasiyo na athari katika maisha halisi ambayo mara nyingi huwakilishwa katika kazi za kufikirika, (fantasia) na majaribio, au zile za kutoa taswira ya kinabii ya baadaye, pamoja na fasihi zinazoelezea uzoefu wa daktari katika kutibu magonjwa mbalimbali, fasihi hizi hujulikana kama wasifu wa daktari na changamoto anazozipitia katika kazi yake, vilevile vipengele vya ugonjwa katika fasihi nipale ambapo ugonjwa ni sehemu ya maisha ya kawaida ya binadamu, lakini si msingi wa kazi wala haitengenezi muktadha wa jumla wa kazi hiyo.

Kwa msingi wa utafiti huu, fasihi ya maradhi inaweza kugawanywa katika makundi mawili kuu, kulingana na mtazamo wa kimuktadha na kimaudhui. Mgawanyo huu unasaidia kufafanua kwa kina jinsi magonjwa yanavyoakisiwa katika kazi za kifasihi.

- Fasihi ya milipuko – ambayo ni kazi ya kifasihi inayojadili ugonjwa unaosambaa kwa haraka na kuathiri watu wengi katika jamii kwa muda mfupi kama vile (UVIKO 19), ikionyesha athari zake katika jamii na mbinu za kukabiliana nao.
- Fasihi ya magonjwa– ni ile fasihi ambayo ugonjwa ni mada kuu na msingi wa matukio na wahusika, ikiwa ugonjwa huo ni wa kuambukiza kama vile (UKIMWI), au usioambukiza kama vile ugonjwa wa saratani, ambapo ugonjwa huo ni dhamira kuu ya kazi ya fasihi na unaathiri jamii kwa ujumla.

Katika utafiti huu, tunajikita katika aina ya pili ambayo ni fasihi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza – inayojadili tatizo linaloikumba jamii kutokana

na janga kubwa la kiafya. Mfano tuliouchagua kuuwakilisha mtazamo huu barani Afrika ni ugonjwa wa UKIMWI (AIDS).

**Fasihi ya kielemu:**

Ni muhimu kutofautisha kati ya aina mbili za fasihi zinazotumia istilahi ya fasihi ya shule. Aina ya kwanza ni ile inayoelezea masuala ya watoto katika shule au vyuo vikuu kupitia maisha yao na tabia zao katika mazingira ya kielimu kama vile riwaya ya First time at Melory Tower ambayo inaelezea maisha ya wanafunzi katika mabweni yao (Blyton, 2016) na hii huitwa kwa Kiswahili Fasihi ya mazingira ya elimu. Aina ya pili ni fasihi inayofundishwa shuleni na huchaguliwa kutoka katika aina mbalimbali za kazi za kifasihi na kuwekwa kwenye mtaala wa masomo kwa madhumuni ya kielimu kama vile kukuza uelewa wa fasihi na uwezo wa uhakiki na kueneza maadili na desturi katika jamii. Aina hii ya pili ndiyo inayolengwa katika utafiti huu, fasihi teule inayochaguliwa na taasisi za elimu kwa madhumuni ya kufanikisha malengo ya kielimu, kijamii na kisiasa. Fasihi hii hutumia mtindo unaoendana na kiwango cha wanafunzi, kwa kuzingatia umri na uwezo wao wa kimawazo. Ni nyenzo muhimu ya kukuza maarifa na maadili miongoni mwa wanafunzi, na pia sehemu ya msingi ya mtaala wa masomo.

Fasihi hii ilianzishwa katika mitaala ya elimu ya Tanzania na wakoloni, na iliendelea kuwepo hata baada ya uhuru, ingawa kazi za fasihi ya Kiswahili zilichukua nafasi ya kazi za fasihi ya Kiingereza za kale ambazo hapo awali zilikuwa sehemu ya fasihi ya shule. Kazi bora za riwaya, tamthilia na mashairi zilizoakisi jamii na utamaduni wake zilichaguliwa kwa makusudi ya kufundishwa shuleni, kwa mujibu wa vigezo maalum vya serikali. Kwa kawaida, uchaguzi huu uliendana na sera na mwelekeo wa serikali katika juhudi zake za uelimishaji na uhamasishaji, hasa katika kampeni zinazohusu afya na kuenea kwa magonjwa. Hii ni kwa sababu " kinyume na hapo awali ambapo maradhi mengi yaliathiri wazee waliopevuka kiumri, miaka ya hivi karibuni, maradhi sugu yamekuwa yakiathiri hata Watoto na vijana"(Kisangau & Kevogo, 2024, p. 31) Kundi lengwa la fasihi hii ni watoto wa shule ya msingi hadi sekondari, ambao ndio kundi linalolengwa na fasihi ya shule. "Fasihi ya watoto ni fasihi ambayo mwega wa kidhamira na kifani umeegemezwa kwenye hadhira ya watoto. Watoto wanaorejelewa katika makala haya ni wale wa umri wa miaka 12-17. Hawa ndio wanaoweza kusoma kazi za fasihi inayowalenga na kuzielewa." (Bakize, 2013, p. 62) Na kwa kuwa bado vitabu vya watoto nchini Tanzania vinapatikana tu kupitia mfumo wa elimu, huku watoto walio nje ya shule wakiwa hawafikiwi na vitabu hivyo,kwani hakuna maktaba maalum zinazohifadhi vitabu vya watoto pekee. jamii nyingi za Kiafrika, hasa Tanzania, bado hazijazoea utamaduni wa kusoma vitabu, ikiwemo vya watoto, havina soko kubwa, kwani watu hawazingatii usomaji wa vitabu isipokuwa

pale wanapokabiliwa na mitihani. Bila mitihani, watu wengi hawapati motisha ya kusoma. (Bakize, 2013, pp. 67–68)

Hii ndiyo sababu serikali imeamua kulenga wanafunzi wa shule katika kutumia fasihi kama njia ya uhamasishaji kwa watoto, hasa katika miradi inayolenga kumaliza vifo vya akina mama na watoto kwa kutokomeza magonjwa kama Malaria, ambayo huathiri zaidi watoto, pamoja na kampeni ya kutokomeza surua kwa watoto na mengineyo. Mojawapo ya juhudi za serikali ni kuchagua kazi za kifasihi zinazojikita katika matatizo ya kiafya yanayowakumba watoto. Njia mojawapo ni kuwezesha ufadhili wa uandishi wa vitabu vya shule na kuandaa makongamano ya kielimu. (Bakize, 2013, p. 66)

Kwa hiyo, kufadhili uandishi wa kazi za kifasihi kwa madhumuni ya kielimu ni jambo linaloendelea nchini Tanzania. Aidha, kuchagua kazi za kifasihi zenye maudhui ya uhamasishaji na malengo ya kijamii kwa ajili ya kufundishwa mashuleni ni jambo la kawaida, na ni lengo la waandishi wengi wanapoandika kazi zao, kwani linawapa fursa ya kusomwa kwa wingi na kupata mapato kutokana na kazi hizo. Kama alivyoeleza Selina Rhobi Chacha, maana ya fasihi ya watoto huamuliwa kwa kuzingatia mambo matatu muhimu: hadhira lengwa, sababu ya kuandika, na mtindo au aina ya fasihi. Hapa hadhira ni wanafunzi wa shule, sababu ya uandishi ni madhumuni ya kufundisha, jambo ambalo linachangia katika kuwasilisha ujumbe moja kwa moja. Mtindo wa fasihi huamuliwa kwa kuzingatia mwelekeo wa taasisi za elimu na miradi yake ya uhamasishaji na mabadiliko ya kijamii. (Chacha, 2016, p. 15)

**UKIMWI nchini Tanzania:**

Tanzania inakabiliwa na magonjwa sugu ambayo yanawakilisha changamoto kubwa ya kiafya kwa wananchi wake, ikiwa ni pamoja na malaria, homa ya matumbo (typhoid), na UKIMWI. Miongoni mwa haya, UKIMWI ndio unaochukuliwa kuwa tishio kubwa zaidi kwa sababu unahusisha masuala ya kimaadili.

Tangu kugunduliwa kwake kwa mara ya kwanza mwaka 1983 katika eneo la Kagera mpakani mwa Uganda, hususan katika kabila la Wahaya, kumekuwa na mitazamo mbalimbali ya kitamaduni kuhusu chanzo chake, hali inayochangia ugumu wa kuukabili. Ugonjwa huu ulihusishwa na tafsiri za kishirikina, kulingana na tamaduni na mila za Watanzania wengi, ambapo magonjwa yalielezwa mara nyingi kuwa ni matokeo ya laana za mababu, mapepo wabaya, au adhabu kwa kuvunja miiko ya kijamii.

UKIMWI ulionekana kama laana iliyoikumba jamii ya eneo hilo, na uliathiri hasa wafanyabiashara na wavuvi waliokuwa wakisafiri kati ya Tanzania na Uganda wakati

wa vita kati ya nchi hizo. Hali hii ilisababisha waganga wa jadi, imani za kishirikina na tiba mbadala kuwa na nafasi kubwa katika kutibu ugonjwa huo, wakionekana kuwa mbadala wa kukubalika kijamii na pia nafuu kwa watu maskini ikilinganishwa na huduma za tiba za kisasa. Mnamo mwaka 1992, mfumo wa afya ulielekezwa kwenye ubinafsishaji, na huduma nyingi za afya zikawa za kulipia, hali iliyofanya wananchi wengi kushindwa kumudu gharama hizo. (Nicolini, 2022, pp. 29–33) Aidha, unyanyapaaji mkubwa uliowakumba waathirika wa UKIMWI ambao walihusishwa na ukahaba au maisha ya maadili yasiyofaa, hili lilipelekea wengi wao kuficha hali zao, jambo lililochangia ongezeko la maambukizi kwa siri. Zaidi ya hayo, ukosefu wa uelewa kuhusu ugonjwa huu na njia za kujikinga ulitokana na mtazamo wa sehemu ya jamii kwamba ugonjwa huo hauwahusu, kwa kuwa unahusishwa na tabia zisizokubalika kijamii, hasa ngono isiyo halali. (Kalumu & Kevogo, 2024, p. 31)

Kutokana na hali hiyo, mashirika ya serikali na yasiyo ya kiserikali yalianza kushirikiana katika juhudi za kukabiliana na virusi hivyo hatari kupitia kampeni za afya, matangazo na uelimishaji wa moja kwa moja kwa jamii. Miongoni mwa mbinu za kuelimisha umma kuhusu namna ya kujikinga na UKIMWI ilikuwa ni kupitia fasihi. Baada ya muda mfupi, aina mbalimbali za kazi za kifasihi ziligeuka kuwa njia kuu ya kutoa elimu na onyo kuhusu virusi vya UKIMWI. Mashindano ya uandishi wa kazi za kifasihi kuhusu ugonjwa huu yakawa sehemu ya mikakati ya kitaifa ya kupambana na janga hilo.

## Matumizi ya Fasihi kuhusu Ugonjwa wa UKIMWI:

Fasihi ina nafasi muhimu na ya msingi katika jamii, hasa wakati wa majanga na matatizo ya kijamii, kwani huwa kama kipaza sauti kinachoeleza ukweli na kufafanua hatari kwa maneno mepesi na yenye mvuto ambayo ni rahisi kueleweka na kugusa hisia. Hivyo basi, fasihi ni chombo cha kwanza cha uelimishaji hasa katika jamii ambazo hazina upatikanaji mpana wa vyombo vya habari kama magazeti, televisheni, redio au hata mtandao wa kijamii. Katika maeneo ya vijijini, shule zinakuwa mahali bora pa kusambaza taarifa na ujumbe kupitia nyenzo za kielimu wanazopokea wanafunzi. Shule huwakutanisha watoto na vijana, ambao ni kundi muhimu la walengwa wa uelimishaji na pia huwa kiungo cha kusambaza uelewa huo kwa familia zao.

Swala la kuchagua chombo kinachotumika kufikisha ujumbe ni muhimu, na fasihi imekuwa njia yenye ushawishi mkubwa na iliyoenea kwa haraka. Aina zote za fasihi ya Kiswahili zilitumika kueleza na kuonya kuhusu ugonjwa wa UKIMWI hasa kupitia mashairi na nyimbo ambazo zilitumika mapema kwa kuwa ni rahisi

kusambazwa na kukumbukwa, hivyo zikawa miongoni mwa kazi za kwanza za kifasihi kutumika . (Mwilaria, Kobia, & Musyimi, 2024, p. 496)

Aina zote za fasihi zilitumika pia katika mitaala ya elimu "VVU/UKIMWI umetokea mwanzoni katika utanzu wa ushairi, leo umejiingiza katika tanzu zote za fasihi: riwaya, hadithi, mashairi, na tamthilia, kwa kweli tunaweza kusema kwamba dhamira ya VVU/UKIMWI imeumba aina ya fasihi ya pekee. Mwanzoni mwa miaka ya themanini, washairi walikuwa wamejadili kuhusu “ugonjwa usiojulikana” kwa dhima ya kuelewa kumetokea". (Nicolini, 2016, p. 98)

Ingawa ushairi ulikuwa aina ya kwanza ya fasihi kutumika kuelezea UKIMWI, riwaya ndizo zilizotawala zaidi kwa sababu zinakaribiana na maisha halisi ya kijamii. Riwaya nyingi zilianza kuchapishwa zikijadili kwa kina dalili za ugonjwa huo, njia za kujikinga, na sababu za kusambaa kwake, kama vile riwaya ya Kisiki Kikavu ya mwandishi Aldin Kaizilege Mutembei (Mutembei, 2005), na Ua la Faraja ya William Mkufya. (Mkufya, 2004)

Hata hivyo, fasihi ya tamthilia imekuwa na nafasi ya kipekee katika uelimishaji, hasa katika elimu ya fasihi mashuleni, kutokana na uwezo wake wa kuwasilishwa kama maonyesho ya jukwaani, ambayo ni miongoni mwa michezo ya wanafunzi, na hivyo ni rahisi kuyatumia katika muktadha wa uhamasishaji, hasa mashuleni ambapo fasihi inafundishwa. Mbali na hayo, mashindano mengi yalifanyika kuhimiza uandishi wa tamthilia za uelimishaji, kama vile shindano lililoandaliwa na shirika la NACP (National AIDS Control Program) kwa ushirikiano na serikali kupitia programu ya kitaifa ya kupambana na UKIMWI, katika shindano hilo, washairi na waandishi wa tamthilia walishindanishwa kwa kazi zao kuhusu virusi vya UKIMWI, ambapo mwandishi Ibrahim Ngozi alishinda nafasi ya kwanza kwa tamthilia yake ya Ushuhuda wa Mifupa mwaka 1989 . (Nicolini, 2016, p. 99) Tamthilia hiyo ilifundishwa mashuleni wakati huo, lakini kwa sasa haifundishwi tena kutokana na ongezeko la tamthilia nyingi za kisasa zinazozungumzia suala la UKIMWI.

## Mbinu ya Utafiti: Nadharia ya Muktadha (Contextual Approach):

Nadharia ya muktadha ni mbinu ya uhakiki wa fasihi inayozingatia uchunguzi wa mambo yote yanayoathiri uundwaji wa kazi ya kifasihi pamoja na athari yake kwa wasomaji. Mbinu hii huangazia mchango wa mazingira ya nje katika kuzaliwa na kuundwa kwa kazi ya kifasihi, hasa zile kazi zenye madhumuni ya kuelimisha au kuelekezwa kwa hadhira maalum. Kwa msingi huu, mbinu ya muktadha hujumuisha mielekeo mitatu ya kiuhakiki: nadharia ya kihistoria, nadharia ya kijamii, na nadharia ya kisaikolojia, ambazo huunganika pamoja ili kutoa picha kamili ya mazingira ya nje yanayoizunguka fasihi. Uchambuzi na uelewa wa jinsi mazingira haya

yanavyofanya kazi ni jambo la msingi katika uhakiki wa fasihi, kwani kuelewa kazi ya kifasihi “kunapaswa kuwa na msingi wa uelewa wa awali wa asili ya falsafa, mitazamo ya kiitikadi, muktadha wa kitamaduni, historia na mazingira ambamo kazi hiyo ilizaliwa”. (Hammoudin, 2008, p. 183) (Tafsiri kutoka kwa kiarabu)

Hivyo basi, uhakiki wa muktadha hutegemea msingi wa kijamii na utamaduni unaoathiri kazi ya fasihi,“Uhakiki wa muktadha ni mwangaza wa nje unaosaidia kusoma maandishi ya kifasihi kwa kutumia muktadha wa kihistoria, kijamii, na kisaikolojia yanayolizunguka. Ingawa maandishi hutoka ndani ya nafsi ya msanii, bado huathiriwa na mitazamo ya kitamaduni na kihistoria inayomwelekeza msanii. Hivyo basi, muktadha wa nje ni njia muhimu ya kuyaelewa maandishi ya fasihi na kufichua maana zake za ndani”. (Arous, 2019, p. 220) (Tafsiri kutoka kwa kiarabu)

Kwa msingi huo, utafiti huu unalenga kufichua misingi ya kimuktadha inayosimamia tamthilia za kiswahili zinazoshughulikia janga la UKIMWI kwa kutumia uhakiki wa muktadha. Uhakiki huu unategemea mbinu ya kihistoria inayojikita katika maisha ya mwandishi, mitazamo yake na mawazo yake yaliyosababisha kazi hiyo kuandikwa, pamoja na mbinu ya kijamii inayozingatia mazingira ya jamii husika, mila, tamaduni, na desturi ambapo kazi hiyo iliandikwa, na mbinu ya kisaikolojia inayotegemea uchambuzi wa mienendo ya kibinadamu na nafasi yake katika kuelewa na kupokelewa kwa kazi hiyo na hadhira. Misingi hii ndiyo inayounda mfumo wa uelewa wa kazi na malengo yake. Kwa kutumia utafiti wa kimuktadha, tunaweza kutathmini kama lengo la kazi limetimia kupitia athari yake ya kisanaa na kijamii, hasa kwa kundi lengwa la wanafunzi wanaosoma kazi hizo mashuleni, sambamba na kueleza historia ya mwandishi na madhumuni ya kijamii ya kazi hizo kwa ajili ya kuendeleza jamii. Kwa sababu hiyo, utafiti huu unaamini kuwa nadharia ya muktadha ndiyo inayofaa zaidi kutumika katika kazi hii ya utafiti, kwa kuwa inatoa mwongozo wa kuelewa maandiko ya kifasihi.

## 1- Muktadha wa kihistoria:

Kulingana na ripoti ya mwaka 2023 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya UKIMWI (UNAIDS), asilimia ya watu wazima walioambukizwa virusi vya UKIMWI nchini Tanzania ni asilimia 4.7, huku idadi ya watoto walioambukizwa ikikadiriwa kufikia watoto 85,000. Hii inawakilisha jumla ya watu milioni 1.4 wanaoishi na virusi hivyo nchini Tanzania katika mwaka huo huo wa ripoti . (UNAIDS, n.d.)Hali hii inaonyesha kuwa ugonjwa huu ni tatizo la kijamii linalotishia jamii kwa ujumla tangu ulipojitokeza kwa mara ya kwanza katika miaka ya 1980 ya karne iliyopita. Hali hiyo ilizifanya taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kutambua umuhimu wa kukabiliana nalo.

Hata hivyo, changamoto kubwa ni kwamba hadi sasa hakuna tiba madhubuti inayoweza kuutibu ugonjwa huo kikamilifu. Kwa hivyo, kinga na uelimishaji wa jamii vikawa silaha kuu na muhimu zaidi katika kupambana na ugonjwa huu. Jambo hili linaonekana wazi katika tamthilia zitakazojadiliwa na kuchambuliwa katika utafiti huu, ambazo ni: Kilio Chetu iliyoandikwa na Medical Aid Foundation mwaka 1995 . (Medical Aid Foundation, 1995), Orodha ya Steve Reynolds ya mwaka 2006 (Reynolds, 2006), na Mwalimu Rose ya Mghanga F. Ambrose ya mwaka 2007 . (Ambrose, 2007)

**A-** **Tamthilia ya Kilio Chetu:** Tamthilia hii hufundishwa katika shule za sekondari kama sehemu ya kitabu cha fasihi kwa wanafunzi wa Kidato cha 3 na 4 katika mfumo wa elimu ya sekondari nchini Tanzania. Tamthilia hii inafundishwa kwa wanafunzi wa kidato Kidato cha 3, ambao umri wao kwa kawaida huwa kati ya miaka 15 hadi 16, kwa mujibu wa *Tahakiki vitabu teule vya fasihi* kilichoandikwa na Nyangwine, Mhilu, na Kanyuma (2021). kipindi ambacho mara nyingi huanza mahusiano ya kimapenzi. Hii ni hatua muhimu ambayo vijana wanapaswa kuwa na ufahamu wa athari zinazoweza kutokana na mahusiano hayo, hasa yanapoendelea hadi kuwa ya kimwili, jambo ambalo linaweza kuwaweka katika hatari ya kuambukizwa magonjwa hatari kama UKIMWI.

Kwa sababu hiyo, kundi hili la umri linalengwa sana katika kampeni za uelimishaji wa kinga kupitia michezo ya kuigiza shuleni, ambapo tamthilia ya Kilio Chetu hufundishwa na kuonyeshwa. Tamthilia hii ya uelimishaji ina mtindo wa moja kwa moja na rahisi wa uwasilishaji, hivyo ni rahisi kueleweka na kupokelewa na watoto wa umri huo bila ugumu wowote katika kuelewa ujumbe wake.

Tamthilia hii iliandikwa chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam - UDSM) kupitia kitengo cha Parapanda Arts, ndani ya Taasisi ya Masomo ya Kiswahili (Institute of Kiswahili Studies), kilichokuwa chini ya uongozi wa Mgunga Mnyenyelwa, ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Parapanda Arts wakati huo. Mradi huu ulifadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kama sehemu ya Mradi wa Utafiti wa UKIMWI katika mkoa wa Kagera, kupitia shirika lisilo la kiserikali la Medical Aid Foundation. (Nicolini, 2022, pp. 87–89) Tamthilia hii iliibuka kufuatia uchunguzi wa moja kwa moja wa kutokuwepo kwa maarifa ya kina miongoni mwa wanafunzi kuhusu elimu ya afya na kuenea kwa taarifa potofu kuhusu njia za maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Hali hii inaonyesha kwa wazi mchango wa mashirika ya kimataifa katika kusaidia miradi ya ndani barani Afrika kupambana na changamoto za kiafya kwa kushirikiana

na mashirika yasiyo ya kiserikali. Shirika la Medical Aid Foundation linachukuliwa kama mwandishi wa kisheria wa tamthilia hii, ambayo haikulenga sana katika thamani ya kifasihi bali katika kutoa maarifa na tahadhari kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa wanafunzi wa shule.

Lengo la kielimu ndilo lilikuwa msingi wa uandishi wa kazi hii, jambo linaloeleza kwa nini tamthilia hii ina upungufu katika mtiririko wa hadithi (ploti) na inaeleza ujumbe kwa njia ya moja kwa moja, licha ya hayo, tamthilia hii imekuwa maarufu sana kwa sababu ya urahisi wake wa kueleweka na kueleza dhima yake kwa wanafunzi. Tamthilia hii ilichapishwa na Mkuki na Nyota Publishers Ltd, Dar es Salaam, ambao ni mojawapo ya wachapishaji maarufu wa kazi za kifasihi na mfululizo wa vitabu vya tamthilia nchini Tanzania.

**B-** **Tamthilia ya Orodha:** Tamthilia hii hufundishwa katika ngazi ya elimu ya sekondari katika kitabu cha fasihi kwa wanafunzi wa Kidato cha 3 na 4 nchini Tanzania pamoja na tamthilia ya Kilio chetu, lakini imetengwa mahsusi kwa ajili ya Kidato cha 4, ambapo mara nyingi umri wa wanafunzi ni kati ya miaka 16 hadi 17, yaani katika hatua ya juu zaidi ya tamthilia iliyotangulia. Hali hii inaonesha maendeleo ya kielimu pamoja na maendeleo ya mtindo wa fasihi kutoka kwenye uwasilishaji wa moja kwa moja wa kazi rahisi ya kielimu hadi kwenye tamthilia ya Tanzia-ramsa ( Tragicomedy) inayojadili suala la UKIMWI kwa mtazamo wa ucheshi kupitia matukio ya kuchekesha yanayoonyesha janga kwa namna ya kuvutia. Aina hii ya tamthilia huonyesha mabadiliko ya mkondo wa matukio ya tamthilia na kuifanya ya kipekee na kusisimua, na hili hufanikishwa kupitia hali ya majuto au toba ya makosa yaliyofanywa na mhusika mkuu. Kwa kawaida, tamthilia hii huishia kwa furaha, kinyume na kazi nyingi za tamthilia za tanzia ya urasimi ambazo huakisi mitazamo ya tamthilia kuhusu mhusika mkuu aliyejutia na kurejea katika njia sahihi, hata kama mwisho wake unaweza kuwa mbaya, lakini huleta matumaini na furaha kwa watu wengine ambao tamthilia inalenga kuwasaidia kuvuka matatizo yao na kuelewa mazingira yanayosababisha matatizo hayo.

Aina hii ya tamthilia ya Tanzia-ramsa haijaenea sana katika fasihi ya Kiafrika, kama alivyosema Mataro: "Utanzu huu wa tamthiliya sio maarufu miongoni mwa wanatamthiliya wa Kiafrika." . (Chacha, n.d.) Waandishi wa Kiafrika hupendelea kuonesha matatizo ya kijamii kwa mtazamo halisi wa kifasihi wa kijamii na unaoonesha picha halisi ya jamii. Lakini aina hii ya tamthilia ya Tanzia-ramsa imeenea zaidi katika fasihi ya Ulaya, na kwa sababu mwandishi wa tamthilia hii ni Mwingereza aitwaye Steve Reynolds, aliyekuwa mwalimu wa tamthilia na sanaa za maonyesho kwa miaka 21 katika sehemu mbalimbali duniani, alipofika miaka 36

aliamua kuhamia Tanzania ambako alifanya kazi kama mkuu wa idara ya sanaa bunifu katika Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (International School of Tanganyika). Alianzisha warsha na vikundi vya tamthilia kwa vijana vilivyoitwa Dar es Salaam Young People's Theatre, na aliandika kazi mbalimbali za kifasihi kwa ajili ya kuigizwa kwenye jukwaa hilo, zikiwemo Vibaka na The List, ambayo baadaye ilitafsiriwa kwa Kiswahili kwa jina la Orodha na Saifu D. Kiango, (Shulevalley, 2024) Lengo la tamthilia hii lilikuwa kuonesha tatizo la UKIMWI kwa namna ya kichekesho ili kuwasaidia vijana kuepuka maambukizi na kujikinga. Tamthilia hii ilipokelewa kwa mafanikio na kuwavutia vijana kutokana na mtindo wake wa kuvutia wa kuwasilisha janga la UKIMWI kwa mtazamo mpya wa Tanzia-futuhi katika jukwaa la elimu nchini Tanzania. Hali hiyo ilichangia tamthilia hiyo kuchaguliwa kufundishwa mashuleni, hasa kwa kuwa mwandishi wake Steve Reynolds alikuwa na uhusiano na mfumo wa elimu nchini humo.

Hatutaingia katika mjadala kuhusu iwapo kazi hii haiwezi kuhesabiwa kuwa ya fasihi ya Kiswahili kwa sababu mwandishi wake si Mswahili na kazi iliandikwa awali kwa lugha ya Kiingereza. Hii ni kwa sababu inachukuliwa kuwa fasihi iliyotafsiriwa kwa Kiswahili, ingawa tamthilia hii iliandikwa mahususi kwa ajili ya jamii ya Waswahili na kwa maonyesho ya shule nchini Tanzania. Jambo la msingi katika utafiti huu ni kwamba ni fasihi ya shule inayofundishwa kwa wanafunzi wa Kitanzania kwa lugha ya Kiswahili, na inazungumzia virusi vya UKIMWI.

Tamthilia hii ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2006 na shirika la uchapishaji nchini Tanzania liitwalo Macmillan Aidan, na toleo jingine la tamthilia hiyo lilitolewa tena mwaka 2021 na shirika la uchapishaji la APE Network, na inapatikana pia katika baadhi ya maduka ya mtandaoni nchini Tanzania kama Elitestore.

**C- Tamthilia ya Mwalimu Rose:** Tamthilia hii hufundishwa katika ngazi ya elimu ya sekondari ya juu (high school) kupitia kitabu cha pili cha mtaala wa fasihi kwa wanafunzi wa Kidato cha 5 na 6 katika elimu ya sekondari ya juu nchini Tanzania, ambapo wanafunzi wa kiwango hiki cha elimu huwa na umri kati ya miaka 18 hadi 20. (Masebo & Nyangwine, 2018) Huu ni umri wa ukomavu wa vijana wanaokamilisha elimu ya sekondari na wako katika hatua ya kabla ya kujiunga na vyuo vikuu, hivyo inatarajiwa kuwa na uelewa mpana na hali ya utambuzi wa juu, jambo linalohitaji kazi ya kifasihi inayoelezea kwa undani kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Haya yote yamepatikana katika kazi ya Mwalimu Rose iliyoandikwa na Mghanga F. Ambrose ambaye aliwasilisha tamthilia ya kijamii iliyojaa huzuni na uhalisia wa changamoto zinazoikumba jamii ya Kitanzania. Mada ya ugonjwa wa UKIMWI ilijadiliwa ndani ya muktadha wa matukio mbalimbali ya kifasihi kwa

kina, si kwa mtazamo mmoja na wa wazi kama ilivyokuwa katika tamthilia zilizofundishwa katika ngazi za chini za elimu.

Ufanisi huu umetokana pia na ukweli kwamba mwandishi huyu ni mtunzi wa Kitanzania aliye mahiri katika fasihi ya Kiswahili na mshauri wa uandishi na uhariri wa vitabu vya watoto. Aidha, ni mtafiti wa lugha katika Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), na pia ameshiriki katika kuhariri vifaa vya kufundishia kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na kukuza ujuzi wa lugha kupitia vitabu vifuatavyo: Uchopekaji wa Masuala Mtambuka katika Mtaala wa Elimu ya Awali, na Moduli ya Kufundisha Kuandika. (Ambrose, 2007, back cover)

Mbali na hayo, anafanya pia kazi za kitaaluma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Historia hii ya kifasihi na kitaaluma imemuwezesha kuandika kazi ambayo si tu yenye lengo la kuelimisha moja kwa moja, bali ni kazi kamili ya kifasihi inayofaa kwa kundi la umri wa juu zaidi. Tamthilia hii huwapa wanafunzi fursa ya kujadili kwa undani mambo ya kijamii yanayowakabili kwa mtazamo mpana zaidi, na vilevile inaweza kuoneshwa mbele ya hadhira ya jumla, si tu kwa matumizi ya maonesho ya shule.

Tamthilia hii ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2007 na kampuni ya uchapishaji ya Macmillan Aidan nchini Tanzania, kampuni inayojihusisha na uchapishaji wa kazi za kifasihi zenye lengo la kielimu.

## 2- Muktadha wa Kijamii :

Ikiwa muktadha wa kihistoria ndio kichocheo cha kuzaliwa kwa kazi za kifasihi zinazohusu maambukizi ya magonjwa, basi muktadha wa kijamii ndio unaoeleza sababu ya kuibuka na kuenea kwa janga hilo. Hii ni kwa sababu fikra za kijamii na dhana za kimitholojia ni miongoni mwa sababu kuu za kuenea kwa magonjwa haya, jambo ambalo hujitokeza wazi katika uchambuzi wa muktadha wa kijamii wa tamthilia. Kazi hizi za fasihi huwakilisha aina ya dystopia ya magonjwa kwa kutumia mbinu za usimulizi ili kuonyesha athari za huzuni zitokanazo na magonjwa yanayosababishwa na mitazamo potofu ya kiitikadi au maovu ya kijamii, kimaadili na kisiasa. Hivyo basi aina hii huonyesha mvutano kati ya binadamu na ugonjwa, na kati ya binadamu na hali ya jamii anayoishi kama vile matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kimaadili, hali ambayo huonesha unyonge wa mwanadamu mbele changamoto za maisha . (Al-Qammi, 2021, pp. 943–946)

Kwa ujumla, kushughulikia matatizo ya kijamii na uhalisia wa maisha ni miongoni mwa mitindo ya kifasihi iliyoenea zaidi katika fasihi ya Kiswahili na ya Kiafrika.

Kwa sababu hiyo, mada ya janga hujadiliwa ndani ya muktadha halisi wa kijamii unaowasilisha tatizo hilo kwa kuonyesha matatizo mengine ya kijamii yanayosababisha au kuambatana nalo, ili kuwasaidia hadhira kufahamu mazingira yaliyochangia kuibuka kwake. Mtazamo huu unakaribiana sana na ule wa tamthilia ya kishujaa ya kijamii (epiki) inayolenga kuiamsha hadhira kimtazamo kuhusu tatizo badala ya kumfanya ajihusishe kihisia na tukio. Hivyo, lengo kuu la kazi hiyo ya kisanii ni kutoa onyo na kuonesha hatari za tatizo hilo.

Hali hii ndiyo iliyomfanya Cristina Nicolini katika utafiti wake juu ya tamthilia za Kiswahili zinazozungumzia ugonjwa wa UKIMWI azichambue kwa kutumia nadharia ya ukengeushi (alienation theory) ya mwandishi wa tamthilia Bertolt Brecht, ambaye aliamini kuwa tamthilia ni chombo cha kuelimisha jamii kwa kuhamasisha fikra na uchambuzi wa kina kutoka kwa hadhira

Hivyo basi, tunaona katika tamthilia zinazochunguzwa kuwa na muktadha mbalimbali ya kijamii, ambapo kila tamthilia imelenga muktadha wa kijamii mahususi unaoendana na malengo ya mwandishi wake na unaofaa kwa kundi la umri lililokusudiwa, kama ifuatavyo:

> **A- Tamthilia ya Kilio Chetu:** Tamthilia hii imejikita katika muktadha wa kijamii unaohusiana na fikra za kifamilia pamoja na imani za jadi kuhusu malezi katika jamii za Kiafrika, ambazo huona kuwa si jambo linalokubalika kuzungumza kuhusu mahusiano ya kingono kwa watoto au hata vijana wa rika la kubalehe. Mtazamo huu unawafanya watoto na vijana kuwa katika hatari ya kupokea taarifa zisizo sahihi kuhusu masuala haya, na kwa njia potofu.

Ingawa fikra hii ni mpya kwa jamii ya Kiafrika, imepokelewa kwa mapana kwa kuwa inaongeza uelewa miongoni mwa wanafunzi walioko katika umri wa kuelewa kuhusu magonjwa ya zinaa yanayohusiana na mahusiano ya kingono miongoni mwao. Magonjwa haya huenea kwa kasi miongoni mwa vijana hasa pale ambapo hamna msingi wa kidini wala uangalizi wa kutosha kutoka kwa familia.

Ueneaji wa mtazamo huu ulisaidiwa na mawazo ya Ulaya yaliyosisitiza umuhimu wa elimu ya mahusiano na hitaji la kufundishia watoto. Dhana hii ilitangazwa kwa nguvu na shirika la serikali la Marekani linalojihusisha na kusaidia maendeleo na kusaidia nchi zinazoendelea duniani kote (USAID - Wakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa) kupitia ufadhili wa tamthilia hii, jambo lililoonekana wazi kupitia utangulizi ulioandaliwa na Bibi Vivian J. Mmari., Makamu Mwenyekiti wa Medical Aid Foundation, ambaye alieleza kuwa tamthilia hii ni kilio kutoka kwa watoto

wenyewe, wakiwasihi wazazi wao kufafanua mahusiano ya kingono kwa njia sahihi na kuanzisha mazungumzo ya wazi kuhusu masuala haya. Kama alivyoelezea katika mwanzo wa tamthilia;

" KILIO CHETU ni tamthiliya nzito inayojaribu kuvunja ukimya mkubwa " uliotawala miongoni mwa jamii katika kutatua matatizo makubwa ya kijamii ambayo chimbuko lake ni uhusiano wa kijinsia. Katika tamthiliya hii watoto wanatoa sauti ya jitimai iliyojaa masononeko na shutuma dhidi ya wazazi, "(Medical Aid Foundation, 1995, introduction)

Inasisitizwa kuwa tatizo halisi katika kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI miongoni mwa watoto ni mila na desturi za kijadi zinazohusiana na dhana ya aibu katika mafundisho kuhusu masuala ya ngono kupitia mazungumzo kati ya wazazi na watoto. Hivyo basi, tamthilia hii, kama ilivyoelezwa na watayarishaji na wafadhili wake wenye mtazamo wa Magharibi unaokumbatia dhana ya malezi ya kisasa, ilikuja kama jaribio la kuvunja ukimya huo, kwa kuwa wanaamini kuwa hiyo ndio njia sahihi ya kutatua tatizo hili miongoni mwa watoto.

Tamthilia ilichagua mbinu ya mawasiliano ya moja kwa moja, kwa maelezo ya wazi na mtindo rahisi usiohitaji tafsiri nyingi ili kufikisha wazo hili kwa urahisi kwa wanafunzi na wazazi. Hili lilifanyika kupitia mlinganisho wa wazi kati ya wahusika wawili: MAMA SUZI na BABA JOTI wanaokataa elimu ya mahusiano kwa watoto wao na kushikilia mila na taratibu za zamani katika malezi. Mtazamo huu ulisababisha uhusiano wa kingono kati ya SUZI na JOTI, uliompelekea JOTI kufariki dunia, SUZI kubeba mimba na kuambukizwa UKIMWI.

Kinyume chake, tamthilia inaonyesha fikra ya BABA ANNA na MJOMBA, wanaowakilisha mtazamo wa mwangaza unaounga mkono elimu ya mahusiano kwa watoto ili kuwalinda dhidi ya kuingia katika mahusiano ya kingono yanayoweza kuwaweka hatarini kwa magonjwa ya zinaa. Hivyo basi, ANNA anafanikiwa kujilinda na kukataa ombi la kuingia katika uhusiano wa mwenzake MWARAMI, kutokana na uelewa alioupata kupitia majadiliano ya wazi na wazazi wake kuhusu masuala hayo.

Mbinu ya kutengeneza chuki dhidi ya wahusika wanaoshikilia fikra potofu za jadi ilitumika kwa kuonyesha wahusika hawa kama wale wanaowapiga na kuwaadhibu watoto wao kwa ukatili bila mazungumzo au kuelewana, kama vile alivyooneshwa Baba Joti.

" Mh, ee bwana we! Nyie ndiyo mnaharibu watoto. Kiboko na mjeledi ndio dawa yake. Wakati wao bado. Na toka lini jamii yetu ikaruhusu kukalishana kitako na

vitoto ukavieleza habari za ngono?" (Medical Aid Foundation, 1995,p.12)

Mtazamo huu umeunganishwa pia na wahusika wanaoshikilia kwa nguvu mila na desturi asilia, kama vile Mama Suzi, ambaye anaegemea maadili ya kijamii yanayokataa maneno machafu yaliyoandikwa kwenye mavazi, na anashikilia mizizi ya kitamaduni kwa uthabiti, kama inavyoonyeshwa katika sehemu ifuatayo:

"Tumebomoa ghala imara ya kuhifadhia maadili yetu. Ghala tuliyoijenga kwa miti yetu ya asili. Na sasa tunatukuza ghala iliyojengwa kwa miti dhaifu ya kigeni. Miti inayoungua kama mabua. Miti ambayo haipatikani kwa urahisi hapa kwetu. Miti ambayo gharama zake hatuzimudu. Sijui tunaelekea wapi!" (Medical Aid Foundation, 1995,p.9)

Hapa inaonekana wazi kuwa msimamo wa Mama Suzi wa kushikilia mila na tamaduni zake za zamani pamoja na imani zake thabiti, na kukataa kabisa kuziacha fikra hizo kwa kuziona kama mti imara usioyumbishwa, kinyume cha mawazo ya kigeni anayoyatazama kama dhaifu na rahisi kuvunjika kama nyasi kavu,hilo lilimpelekea kuangamia na kuwa chanzo cha binti yake kuambukizwa UKIMWI na kupata

ujauzito wa nje ya ndoa. Hili ni dokezo kuwa kushikilia mila za zamani bila kuendana na maendeleo ya kisasa, au kupokea mawazo ya kigeni, kunaweza kupelekea madhara makubwa kwa mtu binafsi na kwa jamii kwa ujumla.

Kinyume chake, wahusika wanaokubali mabadiliko, mwangaza wa maarifa, elimu ya mahusiano na mawazo ya kigeni , kama Baba Anna waliweza kuwalinda watoto wao dhidi ya kuingia kwenye mahusiano ya kingono ambayo yangeweza kuwaangamiza, baada ya kuwapa elimu na mwongozo sahihi.

Athari ya muktadha wa kihistoria unaohusiana na wafadhili na wawezeshaji wa kazi hii kutoka mataifa ya Magharibi inaonekana wazi katika namna walivyoshughulikia na kuelewa muktadha wa kijamii wa Kiafrika. Hawakutosheka tu na kuhamasisha dhana ya elimu ya mahusiano mashuleni kama suluhisho la kupambana na kuenea kwa UKIMWI, bali pia walionyesha dharau kwa mila na imani za jadi za jamii ya Kiafrika na kudokeza kuwa dini haina uwezo wa kutatua tatizo hili. Badala yake, walisisitiza kuwa suluhisho liko katika taasisi za kielimu na mashirika yenye malengo ya kuelimisha, kama alivyonukuliwa MJOMBA katika mazungumzo yafuatayo:

"Watu wanasingizia mila na desturi, na wengine oo.. dini zinakataza. Mbona hizo taasisi zimekuwepo miaka yo yote lakini madhara yatokanayo na zinaa ndiyo kwanza

yanaongezeka. Dini na mila zimeshindwa kumaliza tatizo hili"(Medical Aid Foundation, 1995,p.14)

Ingawa tamthilia ilipunguza nafasi ya utamaduni na ustaarabu wa Kiafrika katika kukabiliana na janga la UKIMWI, bado ilitumia mbinu za masimulizi ya kijadi zinazohusiana na kutumia mtambaji kama msimulizi halisi anayeingia katika muktadha wa matukio. Hii ni mbinu ya kitamaduni ya jamii ya Kiafrika ambayo huwaheshimu warithi wa masimulizi na kuwaona kama wasomi wa jamii, kwa kuwa wana maarifa, hekima na urithi wa kitamaduni.

Hivyo basi, tamthilia ilianza kwa maneno ya kuvutia yaliyotolewa na mtambaji . kisha ikatumia mhusika huyo kwa ajili ya kutoa mwelekeo wa moja kwa moja na kuunga mkono wazo kuu la tamthilia, ambalo ni kutangaza umuhimu wa kufundisha elimu ya mahusiano majumbani na mashuleni. Hili lilionekana wazi kupitia maneno ya MTAMBAJI alipokuwa akielezea hali ya watoto:

"Wapo katika giza nene. Wanashindwa kutofautisha kati ya puto na kondomu. Wazazi wanaliona tatizo hili lakini hawapo tayari kuwapambanulia. Eti mila inakataza. Waongo! Waongo wakubwa. Mbona historia inatueleza kuwa taasisi za jando na unyago kabla ya ukoloni, zilifundisha tendo la ndoa na maisha kwa ujumla wakati wa ndoa. Wazandiki wakubwa. Mila zetu hazikukataza kutoa mafunzo ya elimu ya jinsia bali zilikuwa zikitolewa katika maeneo na nyakati maalumu. Wakoloni na vibaraka wao ndio wanaostahili kulaumiwa. Wakoloni walipiga vita jando na unyago wakidai eti ni ushenzi. Ni ushenzi gani huo?" (Medical Aid Foundation, 1995,p.16)

Mazungumzo haya yanawakilisha njia ya ujanja ya kumshawishi mtazamaji wa Kiafrika kukubali mtazamo wa Kimagharibi kupitia matumizi ya mazungumzo yanayotolewa na mtambaji mwenye busara, ambaye ni kipenzi cha jamii. Hii ni mbinu inayosisitiza kwamba mila na desturi za Kiafrika zinakubali elimu ya mahusiano kwa watoto, kwa kuwa zinatambua umuhimu wa kuwalinda watoto wa kike na wa kiume. Vilevile, tamthilia imetumia chuki ya Mwafrika kwa mkoloni kwa kumweka kama chanzo cha kukosekana kwa mwangaza wa elimu ya mahusiano kwa watoto, kwa kuwa aliwaacha gizani. Hii ni hila nzuri ya kishawishi iliyotumiwa na mwandishi wa kazi hii ili kuwasilisha taarifa anazotaka kuishawishi hadhira kupitia sauti ya mhusika anayependwa, na wakati huo huo kuhusisha mawazo ambayo anataka kutupilia mbali na mhusika asiyependwa na hadhira. Ni mbinu rahisi na ya moja kwa moja inayoendana na mtindo wa wazi wa tamthilia hii.

**B- Tamthilia ya Orodha:** Tamthilia hii inaelezea miktadha yote ya kijamii inayoweza kuwa chanzo cha kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI katika jamii ya Waswahili kwa namna ya kihoja na yenye busara. Inasimulia kisa cha mhusika

mkuu, Furaha, msichana wa kijijini anayeishi katika kijiji ambacho wakazi wake hawana uelewa kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, dalili zake wala njia za kujikinga nao. Kutokana na hali hiyo, Furaha aliambukizwa ugonjwa huo bila kujua kuwa kujamiiana bila kutumia kinga kama kondomu kunaweza kusababisha maambukizi.

Tamthilia hii pia inazungumzia suala la umasikini kama mojawapo ya sababu za kijamii zinazopelekea watu kuingia katika hatari ya kupata ugonjwa huu, kwani wasichana hukubali kufanya mapenzi bila matumizi ya kinga ili tu kupata mahitaji yao ya kifedha. Hii ndiyo njia ambayo Mary aliitumia kumshawishi rafiki yake Furaha kufanya mapenzi na Bw. Ecko, mmiliki wa baa, mzee kwa umri, ili apate burudani na pesa. Mwandishi ametumia dhana ya (sugar daddy) msamiati wa Kimagharibi unaomaanisha mzee tajiri anayekuwa na mahusiano ya kimapenzi na wasichana wadogo huku akiwapatia mahitaji yao,

sababu hii ni miongoni mwa zile maarufu zaidi zinazochangia kuenea kwa UKIMWI katika jamii masikini kama ile ya Waswahili. Hata hivyo, mwandishi anawasilisha mtazamo mpana wa kiuchambuzi na kitamaduni unaoonesha sababu nyingine zinazopelekea ugonjwa huu kama vile kuamini watu wasiostahili kuaminiwa hata kama wana nafasi ya heshima ya kidini, kama viongozi wa dini ambao huenda wakawa wachochezi na waeneza maovu, na hivyo hawastahili kuaminiwa kwa upofu wa jamii. Katika tamthilia, Padri James anatajwa kama mfano wa aina hii.

" mimi pia ni mwanadamu! Mahitaji yote haya ya mwanadamu: peke yangu katika jumuiya hii. Nafanya kile niwezacho kufanya... na bado, kwangu yaelekea kwamba alikwishabikiriwa, kwa hiyo ingeleta tofauti gani? Nilidhani pengine hata ningaliweza kumliwaza? Lakini mtu lazima awe mwangalifu... katika jumuiya ndogo namna hii... taarifa husafiri... wakati wote... kitu fulani huropokwa"(Reynolds, 2006, p.10)

Mwandishi anaeleza kupitia monolojia ya ndani ya Padri James kuwa hakuna mtu mtakatifu kabisa, hata viongozi wa dini, kwani hakuna aliyekamilika au yuko juu ya dhambi. Hivyo basi, mtu yeyote hapaswi kuaminiwa kabisa kwa sababu ya nafasi yake ya kidini. Hakuna misingi ya kudumu katika mahusiano, hata ikiwa ni pamoja na viongozi wa dini. Dhana hii inaakisi mtazamo wa kimaendeleo wa Kimagharibi unaoitwa (positivism), ambao haukubali imani zisizo na msingi wa kisayansi na hauungi mkono udhibiti wa viongozi wa dini au dhana ya misingi ya kidini au kitamaduni isiyopingika.

Tamthilia pia inaonesha namna watu wanavyodanganywa na madai ya mapenzi. Salim alidai kumpenda Furaha na kuanzisha uhusiano naye, kumbe alikuwa mtu mdanganyifu aliyemtumia kwa maneno matamu ya mapenzi ili aweze kufanya

mapenzi, kisha akamkimbia alipopata ugonjwa ambao huenda aliupata kutoka kwake, na hatimaye kuishia kufa.

Pia, tamthilia inaangazia uhusiano wa Furaha na Kitunda, kijana mlevi, mvutaji wa bangi na mwenye tabia mbaya, ambaye alimshawishi Furaha kufanya naye mapenzi kwa kutumia ahadi ya kumsafirisha hadi Dar es Salaam, kumpa maisha ya anasa, na kumvutia kwa redio ya (cassette) muziki, na dansi.

Hivyo basi, mwandishi ameonyesha kwa mapana mazingira ya jamii yanayoweza kuwasukuma wasichana kushiriki ngono na watu mbalimbali, aidha kwa sababu ya umasikini na tamaa ya kifedha, au kudanganywa na kuamini viongozi wa dini au wanaume wanaoaminika lakini ni wadanganyifu, au kwa kuvutiwa na anasa, burudani na safari, au kwa kudanganywa na madai ya mapenzi ya uongo. Sababu zote hizi zina athari kubwa kwa wasichana na huweza kuwaweka katika hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Tamthilia inaonya kuwa msichana anayekubali kushawishika kwa njia hizi si msichana mwema, bali anaonekana kuwa na tabia mbaya kama Furaha, ambaye anakimbia nyumbani, hawatii wazazi, anapenda anasa na maisha ya kiholela, hivyo basi, anastahili hatima ya kusikitisha ya kuambukizwa UKIMWI.

Tamthilia inaonyesha namna magonjwa yalivyo ya kawaida katika jamii ya Waswahili kiasi kwamba Furaha anapomweleza baba yake kuhusu hali yake, anasema huenda ni ugonjwa wa malaria, akimaanisha kuwa si jambo kubwa, kwani ni ugonjwa wa kawaida katika jamii. Hili pia linaonekana katika maneno ya Salim anapojaribu kumfariji Furaha kuwa huenda ana malaria, kifua kikuu au magonjwa mengine ya kawaida Afrika, kana kwamba kuugua si jambo la kushangaza katika jamii za Kiafrika. Hata hivyo, hatari ya UKIMWI ni kuwa ni ugonjwa wa kuambukiza,hauna tiba na husababisha kifo.

Tamthilia imeonesha pia kuwa kuna aina tatu za juhudi za kujilinda na UKIMWI ambazo wanajamii walizichukua kama njia ya kukabiliana na ugonjwa huu usiojulikana. Watu matajiri kama Bw. Ecko na Bwana Juma wanaamini kuwa kufanya ngono na mabikira ni njia ya kinga ili kujilinda dhidi ya maambukizi, hata kama ni kwa gharama ya kuwadhulumu wasichana wadogo, ambapo inatajwa kuwa:

Bw. Juma: ....wanasema kwamba kufanya mapenzi na bikira ni tiba ya uhakika

Bw. Ecko: Kweli!

Bw. Juma: Ndiyo... nasikia ni jambo linalopendwa sana Afrika Kusini.

Bw. Ecko: Ndiyo, lakini mtu atajuaje kama msichana yu bikira?

Bw. Juma: Bw. Ecko... iwapo yu kijana kiasi,... huyo ni bikira! (Reynolds, 2006, p.27)

Majadiliano haya yanaonesha ubinafsi na kujipenda kupita kiasi kwa matajiri, ambao huwatumia wasichana wadogo maskini na wasio na elimu ili kujilinda wao binafsi dhidi ya maambukizi ya UKIMWI, hata kama ni kwa gharama ya heshima na utu wa wasichana hao.

Vilevile, tamthilia inaonesha suluhisho lililochukuliwa na Salim, mhusika mwenye elimu, ambaye amesoma Dar es Salaam na ana maarifa kuhusu njia za kujikinga na UKIMWI. Kwa sababu hiyo, alitumia kondomu wakati wa kufanya ngono ili kujilinda dhidi ya maambukizi. Ingawa alimdanganya Furaha kwa madai ya mapenzi, alitumia njia sahihi ya kujilinda, jambo linaloonyesha kuwa alikuwa na ufahamu wa kweli na mantiki kuhusu kinga.

Tamthilia pia inaonyesha mtazamo wa wakazi wa kijiji ambao walihusisha ugonjwa wa UKIMWI na uchawi, na walijaribu kuutibu kwa kwenda kwa waganga wa kienyeji. Mtazamo huu unawakilisha maoni ya watu wa kawaida na wasio na elimu, ambao hawana uelewa wa kiafya wala wa kitamaduni kuhusu ugonjwa huo.

Hivyo, tamthilia zilishughulikia vyema muktadha yote ya kijamii inayosababisha maambukizi na muktadha yote ya kijamii ya kujikinga na maambukizi ndani ya jamii ya Waswahili.hivyo basi mwandishi ameonyesha tofauti za kimtazamo juu ya sababu nan a kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI kupitia makundi tofauti katika jamii kulingana na ufahamu na kiwango cha elimu walichonacho.

**C- Tamthilia ya Mwalimu Rose:** Tamthilia hii inaonesha muktadha kamili wa kijamii kuhusu matatizo yanayoikumba jamii ya Waswahili. Haikuwasilisha ugonjwa wa UKIMWI kwa njia ya kielimu pekee, bali iligusia pia matatizo na hali mbalimbali za kijamii zinazoiathiri jamii ya Waswahili kwa ujumla, ambazo UKIMWI ni mojawapo ya matokeo yake au huenda ni mojawapo ya sababu za kuenea kwake. Hivyo basi, tamthilia hii ni kazi ya kijamii tofauti na tamthilia za awali ambazo zilikuwa za mafunzo ya moja kwa moja na za tahadhari. Tamthilia hii inaweza kuainishwa kama aina ya Tamthilia tatizo (Problem play) kwa sababu imejadili matatizo mbalimbali ya kijamii.

Tamthilia imegusia nafasi ya pombe na ulevi katika kusambaratisha familia. Imeonyeshwa kuwa Mwalimu Majaliwa alikuwa mlevi wa pombe, mpenzi wa baa na marafiki wa kike, jambo ambalo lilisababisha familia yake kuyumba kiuchumi na kushindwa kutimiza mahitaji ya watoto wao. Hali hii huenda ikawa mojawapo ya sababu zilizomsukuma mkewe kuanzisha uhusiano wa kimapenzi na Bwana Makomango, ambaye ni mkuu wake kazini.

Hivyo basi, usaliti ni muktadha mwingine wa kijamii uliooneshwa kupitia kwa Mwalimu Rose, ambaye alimsaliti mumewe kwa sababu zinazohusiana na kujipendekeza kwa uongozi ili kupata manufaa kazini kutoka kwa bosi wake, au kutokana na umasikini, kwani alimuomba fedha kama masharti ya usaliti huo au kama njia ya kulipiza kisasi kutokana na ulevi wa mumewe, matumizi mabaya ya fedha katika baa na kutotimiza mahitaji ya familia yake.

Msururu huu wa makosa ya kijamii na matatizo ya kifamilia ulisababisha usaliti uliosababisha maambukizi ya UKIMWI kwa Bwana Makomango na kwa Mwalimu Rose. Huyu Bwana Makomango ni yuleyule aliyekuwa akiwahimiza walimu wajiepushe na maambukizi ya UKIMWI katika hotuba yake, huku akiwa amewahamisha walimu kwa dhuluma kwa ajili ya maslahi yake binafsi. Hii inaonesha kuwa hali ya kijamii kwa ujumla ilikuwa sababu kuu ya maambukizi haya ya UKIMWI, ikionyesha kuwa lawama zinaelekezwa kwenye hali ya kiuchumi, maadili katika familia, na matumizi mabaya ya madaraka.

Katika maungamo ya Bwana Makomango, anakiri kuwa alijihusisha na maovu yote anayoweza kuyafanya mtu mwenye madaraka kama vile rushwa, ufisadi, na kuwatendea walimu wake udhalimu pamoja na maovu ya kimaadili kama vile ulevi, uzinzi, kwenda kwa waganga na kuwataka wawadhuru maadui zake, kama inavyoelezwa katika mazungumzo ya tamthilia yafuatayo:

"Nilinywea pombe, nilihongea wanawake na kupeleka kwa waganga. Nilikuwa nawaandikia walimu wangu ripoti mbaya. Nilipokea hongo watoto waache shule wakaolewe na kuchunga ng'ombe. Niliwapa watoto wa shule mimba na kushiriki kutoa mimba, nilihongwa, ili wale waliowapa mimba wasishitakiwe. Nilitoa rushwa kwa wasimamizi wa mitihani ili watoto wa wakubwa wachaguliwe. Nilificha barua za kupandishwa daraja kwa walimu wangu. Niliwazuia kwenda kusoma, nilikuwa mroho wa madaraka. Nilishuhudia uwongo mahakamani. Nilikuwa nakwenda kwa waganga ili nipate na kuendelea kuwa katika madaraka. Niliua kwa uchawi wale waliotaka kutishia nafasi yangu ya madaraka. Nimempa mke wangu huzuni kubwa na mateso makubwa" (Ambrose, 2007, p.70)

Kumkabidhi uongozi mtu asiyefaa ni kosa la kisiasa lililopelekea uharibifu wa mfumo wa elimu kwa wanafunzi na walimu. vilevile Ufisadi katika jamii huanzia kwenye uongozi mbovu unaochochea kuenea kwa dhuluma na mateso ya kijamii hali ambayo hata sheria kali haziwezi kuzuia kabisa. Ingawa sheria ya Tanzania inakataza mahusiano ya kingono na wanafunzi wa shule na kuainisha adhabu ya kifungo cha miaka 30, adhabu hii kali haitekelezwi ipasavyo pale ambapo viongozi wabaya wanahusika katika utoaji wa hongo, kuwapa mimba wanafunzi, kutoa mimba hizo,

na kuwahamisha walimu ili kuficha maovu hayo. Hivyo basi, kumpa mamlaka mtu asiyestahili kunavuruga haki licha ya uwepo wa sheria kali. Tamthilia ilichukua nafasi ya kuangazia matatizo ya kisiasa yanayochochea kuenea kwa maradhi haya, ambayo ni muhimu kama ilivyo kwa matatizo ya kiuchumi na kimaadili katika jamii.

Aidha, tamthilia ilisisitiza mtazamo wa jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, kwa kuonyesha kuwa matibabu aliyopokea Bwana Makomango yalihusiana na tiba za asili , uchawi na waganga wa kienyeji. Aliposhindwa kupona kupitia tiba hizo alikubali pendekezo la Mwalimu Rose kugeukia wahubiri na viongozi wa dini kuomba msaada kwa Yesu katika uponyaji. Hivyo, tukawaona viongozi wa dini wakijitokeza kumtoa pepo mchafu, kama alivyosema Mchungaji:

"Ndugu zangu, pepo hili ni pepo baya sana, pepo lenye nguvu. Pepo hili lina kiburi, tena pepo hili ni maskini lina njaa. Linaendelea kufurahia chakula anachokula ndugu yetu Makoma. Sasa naliamuru, nalipa muda wa siku saba, lazima litoke." (Ambrose, 2007, p.71)

Hili linaonyesha matumizi ya dini na uelekeo wa watu kwenye imani za kiitikadi za kifalsafa zisizo na msingi wa kisayansi, iwe ni kupitia dini au uchawi. Bwana Makomango anakataa kwenda katika hospitali za kisasa kwa ajili ya matibabu, kama alivyosema Mwalimu Rose, hospitali hizo haziwezi kutibu magonjwa kama haya. Hii inaonyesha kuenea kwa ujinga na ushirikina badala ya kutumia tiba sahihi za kisayansi. Vilevile, katika mbinu za kujikinga, Bwana Makomango alidai kuwa anatumia aina maalum ya kondomu kwa ajili ya viongozi, ambayo ni tofauti na ya kawaida na inaweza kutumika mara nyingi kwa usalama. Hizi ni madai yasiyo na msingi ambayo hata Rose alijua hayana mantiki, lakini alikubali kwa sababu yeye ni bosi wake anayemsaidia kifedha na kumsaidia kimaisha. Pia aliahidi kumletea kondomu ya kike kutoka nchi za Ulaya ili kumvutia zaidi na kumpa imani. Madai haya ya uongo na ukosefu wa elimu sahihi katika kinga yalipelekea wao wote kuambukizwa ugonjwa huo.

Wakati huo huo, mke wa Bwana Makomango alichukua hatua ya kujilinda dhidi ya maambukizi baada ya kugundua tabia mbaya za mumewe kwa kujizuia kushiriki naye tendo la ndoa. Hili linaonekana katika mazungumzo kati ya mwalimu Marimba na mwalimu Mende, ambapo alimwelezea mke wa Makomango kama mwanamke mwenye busara na werevu kwa sababu aliweza kujikinga kwa kutokutana kimwili na mumewe. Ni kama mwandishi anapendekeza suluhisho la kihisia kwa mwanamke anayefahamu mwenendo mbaya wa mumewe ili aweze kulinda afya yake. Kwa njia hii, tamthilia imeweza kuchora picha kamili ya kisiasa, kiuchumi, na kimaadili

kuhusu visababishi vya ugonjwa huu katika jamii, na kuonyesha matokeo ya kutojali njia za kinga na uzembe katika matibabu baada ya maambukizi, yote haya yamedhihirika katika kazi hii ya kisanii

**3-Muktadha wa kisaikolojia:**

Muktadha wa kisaikolojia ni kipengele muhimu sana katika fasihi ya magonjwa. Kuonyesha athari za kisaikolojia na mateso anayopitia mgonjwa ni mojawapo wa vipengele muhimu vinavyojadiliwa katika kazi hizi za kifasihi. Kuna kazi nyingi za fasihi ambazo hujikita katika kuonyesha athari hizo za kisaikolojia kwa wahusika waliopatwa na maradhi. Mfano mzuri ni tamthilia ya WIT iliyoandikwa na mwandishi wa Kimarekani Margaret Edson, ambapo mhusika mkuu Vivian aliwasilishwa kupitia muktadha wa kisaikolojia ulioangazia hali yake ya kihisia na kisaikolojia kuhusu ugonjwa wa saratani kwa uzito sawa au zaidi kuliko maelezo ya dalili za ugonjwa huo na matokeo yake.

Kusimama kwenye muktadha huu wa kisaikolojia ni jambo la lazima ili kuelewa mateso ya kibinadamu yanayoambatana na kuugua, ambayo huakisi hali ya ndani ya binadamu. Hali hii huwekwa kwa makusudi katika kazi za fasihi zenye lengo la kutoa onyo au elimu, kwani huonyesha taswira halisi ya kile ambacho mtu anaweza kufikia baada ya kuambukizwa ugonjwa kama vile, huzuni, majuto na hofu na kutupeleka katika hatua nyingine ya muktadha wa kisaikolojia: yaani athari kwa mpokeaji wa kazi hiyo ya kifasihi, iwe ni msomaji au mtazamaji. Hii ndiyo inayowezesha kazi hiyo kutimiza lengo lake na kufikia mafanikio yanayokusudiwa.

A- **Tukianza na Tamthilia ya Kilio Chetu:** Katika tamthilia hii, kipengele cha kisaikolojia kinaonekana kupitia pande mbili. Upande wa kwanza unahusiana na majuto ya wazazi, ambapo tamthilia inaonyesha kuwa walipuuza wajibu wao kwa watoto wao kwa kutowapa elimu kuhusu madhara ya mahusiano ya kimapenzi. Hili lilisababisha watoto wao kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Majuto ya baba yake Joti yanaonyeshwa wazi, kwani licha ya kumpenda mwanawe na kuwa tayari kutumia pesa nyingi kutafuta tiba, anatambua kuwa hakuna faida na anakubali hatima ya mwanawe kwa huzuni kubwa. Mama pia akiangua kilio kwa hisia kali na majonzi anapomwona mtoto wake mkubwa akifa mikononi mwao kutokana na ugonjwa huo hatari.

Taswira hii ambayo inawakilisha mwisho wa moja kwa moja na wa kutarajiwa, inaonyeshwa katika tamthilia kama adhabu kwa wazazi waliokosa kujadili masuala ya elimu ya mahusiano ya kimapenzi na watoto wao.Upande wa pili unaonekana katika majuto ya watoto wenyewe, ambayo ni matokeo ya upuuzaji wa wazazi wao katika ushauri na mwongozo. Hii ilipelekea kuenea kwa taarifa potofu ambazo

watoto walizifuata kwa sababu hawakuwahi kujadiliana mambo haya na wazazi wao. Kwa mfano, Suzy anasema kwamba huwezi kupata mimba kwa kufanya ngono mara moja tu, au kwamba UKIMWI hauwapati watoto bali ni ugonjwa wa watu wazima tu, pamoja na dhana nyingine potofu kuhusu mimba na kuficha ugonjwa wake.

Kilele cha hisia za kisaikolojia kinafikia nyumbani kwa Joti wakati anapokufa, huku Suzy hawezi kujizuia kulia kutokana na hofu na kujihisi kupotea. Hapo ndipo anapomlaumu mama yake kwa kushikilia mila na desturi za zamani, na anaapa kwamba kama wazazi wao wasingepuuza majukumu yao, Joti asingekufa, naye asingepata ugonjwa wala mimba.

." Mama hakuwa radhi kuachana na utamaduni wa kale wa kuweka ukuta baina ya wazazi na watoto katika kujadili mambo haya. Haya ndiyo madhara yake. Naapa kwa Mungu wangu, mimi na Joti tungepata bahati ya kuelimishwa, tusingetumbu...tui (Anaanguka chini)". (Medical Aid Foundation,1995,p.40) kisha Suzy anaanguka chini, jambo linaloonyesha kwa uwazi athari na mshtuko mkubwa alioupata.

Ingawa watoto hawa walikosea kwa kujihusisha na ngono, bado wanaonekana kuwa hawana hatia kwa sababu hawakupewa mwongozo wala elimu sahihi kuhusu masuala ya ngono kutoka kwa wazazi wao.

Mwisho huu wa huzuni na msiba hauleti mshangao kwa mtazamaji kwani tayari ulikuwa unatarajiwa tangu mwanzo wa tamthilia, ambayo inawasilisha wazo lake kwa namna ya moja kwa moja na wazi. Hata hivyo, mwisho huu unazaa matunda ya tahadhari na uelimishaji kwa kundi la wanafunzi wa shule za sekondari, ambao wako katika hatua ya mwanzo wa mahusiano ya kimapenzi.

Hivyo basi, tamthilia hii imekuwa kama kilio cha tahadhari kwa wazazi na watoto,kilio ambacho wanafunzi hukielewa kwa urahisi, hukipokea mashuleni, na hukipeleka kwa wazazi wao majumbani.

B- **Tamthilia ya Orodha:** Tamthilia hii imetumia mbinu ya kisengerenyuma katika kuwasilisha matukio ya mwisho mwanzoni mwa kazi. Inaanza kwa hitimisho lenye mvuto mkubwa, ambalo ndilo msingi wa tamthilia nzima. Tamthilia inaanza baada ya kifo cha mhusika mkuu Furaha, ambapo mama yake anasimama katika mazishi akisoma barua yake kwa kijiji. Barua hiyo iliwatishia wale wote waliokosea naye na kushiriki nae ngono, ambao huenda ndio chanzo cha kuambukizwa kwake virusi vya UKIMWI na kifo chake, kuwa atafichua siri yao.

Hili linawakilisha kilele cha msisimko wa matukio, ingawa ni hatari ya kiuandishi kwa sababu mfuatano wa matukio yanayofuata lazima uwe wa kusisimua zaidi ili

kuendeleza mvuto wa Tamthilia. Ni mbinu ya ujenzi wa matukio isiyotumika sana katika fasihi ya Kiswahili, lakini mwandishi ameweza kwa mafanikio kumvutia usomaji kwa kuunganisha matukio ya kusisimua yenye huruma na hali nyepesi za vichekesho vinavyopunguza uzito wa janga la kifo na hofu ya kufichuliwa kwa siri.

Hii imefanya matukio yaendelee kwa upole unaomvutia msomaji kuendelea kufuatilia hadithi mpaka mwisho usiotarajiwa uliojaa matumaini. Mwisho huu unawakilisha wokovu kwa wale wote waliomuumiza Furaha, kwani aliwapa nafasi nyingine ya kuishi miongoni mwa watu wa kijiji bila kufichua siri yao. Badala yake, aliwasihi kwa maneno ya kibinadamu yaliyojaa matumaini, akiwashauri kutumia kondomu pamoja na kushikilia maadili kama vile uaminifu, uwazi, upendo, msamaha, na tabia njema kwani kushikamana nazo ndio njia ya kuepuka maovu.

Huu ni mwelekeo wa kisaikolojia na ki-dramatiki unaojumuisha mshangao na mabadiliko katika muundo wa hadithi, kwa kutumia matukio ya kihisia yanayogusa hisia kwa urahisi kwa msikilizaji au msomaji, na kumfanya aathiriwe kwa kina na mawazo ya tamthilia.

Tamthilia pia imetoa maelezo ya hali ya hisia ngumu anayopitia mgonjwa wa UKIMWI anayehisi kutengwa na jamii inayomwogopa kwa kuhofia maambukizi. Hali hii imewasilishwa kupitia simulizi ya maumivu aliyopitia Furaha kutoka kwa Salim aliyempenda kwa dhati, lakini alimwogopa hadi kuogopa kumshika mkono au kumkaribia. Hali hiyo ilimvunja moyo Furaha, akabubujika machozi kwa uchungu na kujaa majuto kwa kujiingiza kwa pupa na kimakosa katika mahusiano ya kimapenzi yaliyompelekea kuambukizwa ugonjwa huo.

Kadhalika, mwandishi ameonyesha hali ya wasiwasi na hofu ya kufichuka kwa wale waliofanya uzinzi na Furaha na kusababisha maambukizi na hatimaye kifo chake. Hali hii ya kihisia ilikuja mwishoni mwa tamthilia na ilionyesha wazi kuwa watu wengi walikuwa na hofu juu ya sifa na muonekano wao katika jamii kuliko masuala ya kibinadamu. Haya yaliwasilishwa katika hitimisho la tamthilia kwa ustadi mkubwa.

"Padri anamunyamunya, akiangalia juu, mbinguni. Bw. Ecko anamtazama mkewe – mwanakijiji – ambaye anaangalia nyuma akiwa na uso uliokasirika. Kitunda anajaribu kuonekana ametulia na asiye na hatia. Salim, akiwa nyuma, anaonekana kuwa na wasiwasi na yuko tayari kujitetea". (Ambrose, 2007, p.43)

Tamthilia pia inaangazia tofauti za wahusika katika kukabiliana na hofu na wasiwasi. Kila mhusika anaonyesha mtazamo wake binafsi na namna yake ya kipekee ya kujilinda anapokumbwa na hali ya taharuki. Padri anaonesha mshikamano wake na Mungu kwa kuangalia mbinguni huku akiomba msamaha na kufichwa aibu yake.

Kwa upande mwingine, Bwana Ecko humwangalia mkewe kwa hofu na wasiwasi mkubwa juu ya mshtuko wake na kufikiria usalama wa familia yake.

Wakati huo huo, Kitunda, kijana mlevi aliyejifanya kama mwenye maadili ,anajitahidi kuonekana mtulivu na asiye na hatia ili kuficha udhaifu wake wa kimaadili. Naye Salim, kijana msomi anayedai kuwa na elimu na mapenzi, anaonekana kuwa na msisimko wa kihisia na yuko tayari kulinda heshima yake kijamii kwa njia yoyote, hata kama ni ya kudhuru wengine.

Kwa njia hii, mwandishi anaangazia tofauti wa tabia za kibinadamu na namna binadamu hubadilika wanapojikuta katika hatari au vitisho. Hali hii huibua udhaifu mkubwa wa kibinadamu ambapo kila mtu hujaribu kujilinda au kurekebisha taswira yake mbele ya jamii, hata kama kwa ndani anatambua wazi uzembe wake na upungufu wa maadili katika matendo yake.

C- **<u>Tamthilia ya Mwalimu Rose:</u>** inaonyesha tofauti za kiakili na kihisia kati ya watu wawili waliopata maambukizi ya virusi vya UKIMWI, ikifafanua jinsi hali zao za kisaikolojia zinavyotofautiana baada ya kugundua kuwa wameathirika. Mhusika wa kwanza ni Bwana Makoma, ambaye lengo lake pekee ni kulinda maisha yake na kutafuta tiba bila kujali nani anamtibu au njia ya matibabu , iwe ni kupitia kwa waganga wa kienyeji au viongozi wa kidini. Jambo la msingi kwake ni ubinafsi wake, akidhihirika kama mtu mwenye majivuno, mwenye mamlaka, na anayetamani kumiliki kila kitu ,mfano halisi wa viongozi wabinafsi ambao hujali maslahi yao binafsi pekee.

Kinyume chake, Mwalimu Rose ni mwanamke aliyeanguka katika dhambi ya usaliti na bosi wake ikiwa ni kwa sababu za kifedha kutokana na umaskini, au kijamii kutokana na uraibu wa mumewe mlevi na kutowajibika kwake katika familia, au pengine kutokana na tamaa ya kujipendekeza kwa mamlaka ili apate cheo bora zaidi kazini. Sababu hizi zote zilimpelekea kutenda kosa hilo. Hata hivyo, baada ya kifo cha Bosi huyo na kutambua kuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI, anajawa na majuto makubwa na kujaribu kujiua na akiwa hospitali, anamwita mwanawe na kumwomba msamaha, huku akimtaka amweleze baba yake amsamehe. Anapogundua kuwa mumewe yupo, anamwomba amkumbatie na kumsamehe.

Tukio hili la mwisho linaakisi hisia halisi za majuto na nia ya dhati ya Rose ya kutubu hata kwa njia ya kujitoa uhai, ikiwa kama njia ya kukimbia ugonjwa hatari au kwa ajili ya kutubia usaliti alioufanya kwa mumewe na familia yake. Msomaji au mtazamaji huhisi huruma ya moja kwa moja kwa Mwalimu Rose ambaye, licha ya kosa lake, anatubu na kujaribu kulirekebisha. Kinyume chake, lawama na chuki zote huelekezwa kwa Bwana Makoma, ambaye licha ya kufariki kwa ugonjwa huo, ndiye

chanzo cha maambukizi ya Rose. Katika juhudi zake za kutafuta tiba, anakiri dosari na ufisadi mwingi unaomfanya aonekane zaidi kama pepo kuliko kiongozi.

Kupitia mlinganisho huu wa kisaikolojia, mwandishi anaielekeza hadhira kuwa na msimamo dhidi ya viongozi wabinafsi wasiojali maadili wala jamii. Hivyo basi, muktadha wa kisaikolojia wa tamthilia unahudumia malengo ya kijamii na kisiasa. Mwandishi ametumia janga la UKIMWI kama chombo cha kifasihi kuangazia matatizo ya kijamii na kibinadamu yanayotokana na uongozi mbaya wa kisiasa, hali duni ya kiuchumi, na kuporomoka kwa maadili.

**<u>Hitimisho</u>**:

Inaonekana kutokana na uchambuzi wa miktadha mbalimbali kuwa kazi ya kifasihi hufichua siri kupitia uchambuzi wa muktadha wa kihistoria, kijamii, na kisaikolojia. Siri hizi hufunuliwa hatua kwa hatua kwa kuunganisha miktadha tofauti ili kufichua maana na dhamira iliyofichika. Ingawa tamthilia zote zinakusudia kuelimisha wanafunzi wa shule kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, kila tamthilia ina mtazamo tofauti unaoonyesha sababu na nia zake kupitia uchambuzi wa muktadha wake mahususi, na hii inaonekana wazi kupitia matokeo yafuatayo:

**1- Matokeo ya muktadha wa kihistoria:**

A- Mbinu ya kuwasilisha mada hubadilika kulingana na historia na mazingira ya kitamaduni ya mwandishi. Tamthilia ya Kilio Chetu, iliyoandikwa na Medical Aid Foundation, inasisitiza umuhimu wa elimu ya mahusiano katoka kwa wazazi kwenda kwa watoto na uwazi katika kujadili magonjwa ya zinaa, mtazamo wa maendeleo unaochangiwa na taasisi za kiafya za kimataifa. Wakati huo huo, Orodha huzingatia sababu zinazopelekea wasichana kudanganywa na kuingia katika mahusianoya kimapenzi. mtazamo wa marekebisho kutoka kwa mwalimu wa sanaa wa kigeni anayelenga kuelimisha jamii kuhusu sababu za magonjwa. Naye mwandishi wa Mwalimu Rose huzingatia tatizo hilo katika muktadha mpana wa kisiasa, kiuchumi na kimaadili, akiwa ni mwana wa taifa, anayejua changamoto za jamii yake.

B- Mtindo wa uwasilishaji wa kisanaa hubadilika kulingana na hatua ya kielimu. Hii haimaanishi aibu katika kujadili mada ya UKIMWI, bali mabadiliko ya muundo na ploti ya matukio. Kwa mfano, Kilio Chetu hufundishwa katika ngazi ya chini ya sekondari kwa muundo wake rahisi na wa moja kwa moja. Orodha huoneshwa katika ngazi ya kati ya sekondari kwa mtazamo mpana zaidi, wa maadili na wa kusisimua. Mwalimu Rose hufundishwa katika shule ya juu kabla ya chuo kikuu, ambapo UKIMWI huzingatiwa miongoni mwa matatizo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ili kutoa picha kamili ya jamii.

**2- Matokeo ya muktadha wa kijamii:**

A- Muktadha wa kijamii wa tamthilia zinazoelezea suala la ugonjwa wa UKIMWI hutofautiana kulingana na mtazamo wa jamii husika. Katika tamthilia ya Kilio Chetu, shirika la afya linalowasilisha kazi hiyo linaweka mkazo juu ya wazo la kuwalaumu wazazi wanaokataa kuwafundisha watoto wao elimu ya mahusiano na kukataa mila na desturi za kijamii zinazozuia mazungumzo ya wazi kuhusu mahusiano ya kimapenzi kati ya wazazi na watoto. Kwa upande mwingine, tamthilia ya Orodha haiwalaumu wazazi bali inaonyesha picha ya wazazi wa mhusika mkuu Faraha kuwa ni wazazi wema, na kwamba tatizo liko katika uasi wa vijana kama Farah na tabia zake mbaya . Nayo tamthilia ya Mwalimu Rose inajadili ufisadi wa familia pamoja na jamii kwa ujumla ambayo imejaa umasikini, ufisadi wa kisiasa na mmomonyoko wa maadili. Hivyo basi, sababu za kuenea kwa ugonjwa huu hutofautiana kulingana na mtazamo wa kijamii unaoonyeshwa na mwandishi.

B- Aina ya tamthilia hutofautiana kulingana na malengo ya kisanaa. Kilio Chetu ni tamthilia ya Tanzia ya Kisasa huzingatia kuwa janga ni matokeo ya mitazamo potofu ya jamii, na mhusika mkuu hutoa funzo kwa jamii. Orodha ni Tamthilia ya Tanzia-Ramsa inayowasilisha ujumbe na mwangaza kwa vijana kwa mtindo wa vichekesho vya kusisimua na Mwalimu Rose ni Tamthilia Tatizo – inayoonyesha picha kamili ya matatizo ya kijamii. Hivyo, aina ya tamthilia hutegemea muktadha wake.

C- Mbinu mbalimbali za ushawishi hutumika kufanikisha lengo la kuelimisha wanafunzi kuhusu UKIMWI. Kilio Chetu imetumia mtindo wa masimulizi kwa kutumia msimulizi anayeheshimiwa na kuaminiwa na jamii ili kutoa ujumbe. Orodha inaonyesha miktadha mingi inayopelekea kuambukizwa na miktadha ya kujikinga dhidi ya UKIMWI, kwa hivyo hupanua mtazamo wa mwanafunzi. Mwalimu Rose imetumia mbinu ya kuashiria ugonjwa kama mojawapo ya athari za ufisadi wa kijamii, hivyo kuufanya kuwa alama ya maangamizi yanayosababishwa na uharibifu wa kisiasa, kiuchumi, na kimaadili.

**3- Matokeo ya muktadha wa kisaikolojia:**

A- Katika Kilio Chetu, muktadha wa kisaikolojia unaonesha majuto ya wazazi na watoto, kana kwamba makosa ya wazazi lazima yalipwe na watoto. Hii imewasilishwa kwa mtindo wa moja kwa moja, hali inayofanya kazi kupoteza msisimko kwa sababu mwisho wake unatabirika. Orodha huanza kwa

kuonesha kuwa kifo cha mhusika mkuu kinatarajiwa kutokana na maisha yake ya uasherati. Hata hivyo, kuna msisimko wa orodha inayoweza kufichua waliohusika naye, na mwisho huleta tumaini jipya kwa suluhisho la maadili. Hii humfanya mtazamaji aondoke akiwa ameridhika. Mwalimu Rose imetumia mbinu ya kulinganisha kati ya wahusika wawili wenye UKIMWI. Mmoja anatubu kabla ya kifo na kutafuta msamaha, mwingine anajali kujinusuru bila toba ya kweli. Mbinu hii ya kuchanganya hulenga kuonyesha tofauti za kibinadamu na kuigusa hadhira kihisia.

**Mapendekezo ya Utafiti**:

Imeonyeshwa katika tamthilia zote kuwa matumizi ya kinga (Kondomu) ni njia bora ya kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI, kwa sababu ndio njia pekee ya kujikinga na ugonjwa huu usio na dawa wala tiba, na hili linadhihirishwa pia hata wakati wa sasa serikali imekuwa ikisambaza bure na kuhamasisha matumizi ya Kinga kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Vilevile serikali ya Tanzania inatumia sheria ya kifungo cha miaka 30 jela kwa watu ambao wanajihusisha na matumizi ya kimapenzi na wanafunzi au watoto walio chini ya umri wa miaka 18, Hata hivyo, licha ya juhudi hizi za kiafya na kisheria, changamoto za maambukizi bado zinaendelea. Hivyo basi, utafiti unapendekeza kiuhalisia njia bora zaidi ambayo inatakiwa kutumika ili kuutokomeza ugonjwa huu ni kuimarisha maadili na mafundisho ya dini kwa watanzania kwanzia ngazi ya Familia, mashuleni na jamii kwa ujumla.

**<u>Marejeleo ya Kiarabu (yaliyoandikwa kwa Kiarabu na kutafsiriwa kwa Kiswahili):</u>**


1- العدوي، أحمد. (2013). الطاعون في العصر الأموي: صفحات مجهولة من تاريخ الخلافة الأموية [Tauni katika Enzi ya Umawiyya: Kurasa zisizojulikana]. القاهرة: مركز تراث للبحوث والدراسات.

2- القممي، محروس محمود. (2021). ديستوبيا الوباء في الرواية المصرية: دراسة مقارنة [Dystopia ya janga katika riwaya ya Misri: Utafiti wa kulinganisha]. مجلة كلية الآداب، جامعة الفيوم، (اللغويات والثقافات والمقارنة)، 13(1).

3- بوكاشيو، جيوفاني. (2006). *الديكاميرون* ) [Decameron] صالح علماني، مترجم). دار المدى للثقافة والنشر.

4- حمودين، علي. (2008). الخلفية الفلسفية للمناهج النقدية الغربية [Historia ya kifalsafa ya mbinu za uhakiki wa Magharibi]. الأثر: مجلة الآداب واللغات، 7، جامعة قاصدي مرباح، ورقلة، الجزائر.

5- شيحان، ناصر بن راشد بن. (2022). الوباء في أدب ابن الوردي (ت: 749هـ): دراسة أسلوبية [Janga katika fasihi ya Ibn al-Wardi: Utafiti wa mtindo]. مجلة الدراسات اللغوية والأدبية، العدد 3.

6- عروس، محمد. (2019). النقد السياقي: أسئلتها المنهجية وأسسها الفلسفية [Uhakiki wa muktadha: Maswali ya kimbinu na misingi ya kifalsafa]. مجلة إشكالات في اللغة والأدب، 8(1)، العدد 16، جامعة العربي التبسي، الجزائر.

## Marejeleo ya Kiingereza na Kiswahili:


1- Ambrose, M. F. (2007). *Mwalimu Rose*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

2- Bakize, L. H. (2013). Changamoto zinazoikabili fasihi ya watoto nchini Tanzania. *Kiswahili*, 76. https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kiswahili/article/view/793.

3- Blyton, E. (2016). *First term at Malory Towers*. Hodder Children's Books. (Original work published 1946).

4- Chacha, M. (n.d.). *Moduli ya Kwanza: Nadharia ya Tamthiliya na Drama*. Academia.edu. https://www.academia.edu/36662471/MODULI_YA_KWANZA_NADHARIA_YA_TAMTHIYA_NA_DRAMA

5- Chacha, S. R. (2016). *Uhusiano wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili na umilisi wa kusoma katika shule za msingi, Kasarani, Kaunti ya Nairobi, Kenya* (Master's thesis). Kenyatta University.

6- Cristofer, M. (1993). *The Shadow Box*. New York: Dramatists Play Service, Inc.

7- Kay, A. (2017). *This Is Going to Hurt: Secret Diaries of a Junior Doctor*. London: Picador.

8- Kevogo, A. U., & Kalumu, K. K. (2024). Usawiri wa maradhi sugu yanayodhoofisha mwili katika riwaya teule za Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, 7(2). https://eajss.eanso.org.

9- King, S. (1990). *The Stand: The Complete and Uncut Edition*. New York: Doubleday.

10- Masebo, J. A., & Nyangwine, N. (2018). *Nadharia ya fasihi: Kiswahili 2, Kidato cha 5 na 6* (Toleo jipya). Nyambari Nyangwine Publishers.

11- Mbogo, E. (2002). *Watoto wa Mama Ntilie*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.

12- Mberia, K. W. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

13- Medical Aid Foundation. (1995). *Kilio Chetu*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

14- Mwilaria, R., Kobia, J., & Musyimi, D. (2024). Mitindo ya uwasilishaji wa suala la afya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1).

15- Nicolini, C. (2016). Uhakiki wa tamthilia za Kiswahili zihusuzo VVU/UKIMWI. *Swahili Forum*, 23.

16- Nicolini, C. (2022). A divisive disease: Clashing treatments for HIV/AIDS in Swahili literature. *Kervan International Journal of Afro-Asiatic Studies*, 26.

17- Nicolini, C. (2022). *Clash of Epistemes: Knowledge of HIV/AIDS in Swahili Literary Genres*. Trieste: EUT, Edizioni Università di Trieste.

18- Nyangwine, N., Mhilu, G., & Kanyuma, Y. (2021). *Tahakiki vitabu teule vya fasihi, kidato cha 3 na 4: Nadharia, uhakiki na maswali*. Nyambari Nyangwine Publishers.

19- Porter, K. A. (2023). *Pale Horse, Pale Rider*. New York: HarperCollins, Mariner Books Classics.

20- Reynolds, S. (2006). *Orodha* (S. D. Kiango, Trans.). Dar es Salaam: AIDAN Publishers Ltd.

21- Sacks, O. (1985). *The Man Who Mistook His Wife for a Hat and Other Clinical Tales*. New York: Summit Books.

22- Shulevalley. (2024, March 9). Steve Reynolds Biography. https://www.shulevalley.co.tz.

UNAIDS. (n.d.). *United Nations Programme on HIV/AIDS*. https://www.unaids.org.